





**RIPOTI MAALUM**

## Punda wa kukodi walivyogeuka lulu ukame ukitikisa vijiji

UKURASA 4




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Novemba 20, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581135

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**TATIZO LA UKAME**

# Samia: Tunaadhibiwa kwa makosa yetu

**Awapa** jukumu viongozi wa dini, ataka mabadiliko Sera ya Mambo ya Nje akiteta na mabalozi... *Endelea Ukurasa. 2*



Mgambo wa Jiji la Dodoma wakiondoa meza ya muuza magazeti na kuchukua magazeti katika eneo la Independence jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### UVCCM YAMJIA JUU BASHIRU

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) umemjia juu mbunge wa kuteuliwa, Dk. Bashiru Ali na kumtaka kuomba radhi kutokana na kauli yake aliyoitoa hivi karibuni ya kuonyesha kukerwa na wanaosifia utawala kwa kutumia maneno 'anaupiga mwingi'...

UKURASA WA 7

### TANZANIA YAPIGA HATUA UBORA HUDUMA YA CHOO

WIZARA ya Afya imesema kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita vyoo bora katika ngazi ya kaya vimeongezeka kutoka asilimia 19.5 kwa mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 72.6 mwaka huu..

## Daktari aeleza jinsi alivyochota damu katika mwili wa daktari mwenzake

UKURASA 5

## Zitto aliamsha sakata la gesi asilia

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA, DODOMA JIJI HESABU ZAKAMILIKA UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

## ... Ataka mabadiliko Sera ya Mambo ya Nje

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema hali ya uchumi wa dunia imebadilika kwa kasi kubwa katika muongo mmoja uliopita, hivyo ni vyema Sera ya Mambo ya Nje ikafanyiwa mabadiliko ili kuendana na hali halisi.

Samia aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Mabalozi wa Tanzania wanaowakilisha nchi za nje katika mkutano wa mabalozi hao uliofanyika katika hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar.

Alisema sera hiyo iliandaliwa miaka 20 iliyopita, hivyo kuna mambo mengi yamebadilika duniani na ni vyema kuiangalia upya kama ina mashiko katika mabadiliko ya dunia ili kutoachwa nyuma.

"Kikao hiki kinatupa muda wa kukaa na kutafakari hayo niliyoyasema yakiwamo matishio mapya ya usalama, ustawi wa nchi na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Rais Samia aliwataka mabalozi hao kutafakari majanga ya afya, uhalifu wa kimataifa na mapinduzi ya nne ya viwanda. Pia aliwataka kutafakari mabadiliko ya siasa ya dunia kutokana na kuwapo kwa mivutano baina ya mafahari wa dunia na kuziburuza nchi za Afrika katika migogoro yenye maslahi yao.

"Na athari za migogoro hiyo kwenye bei ya nishati, chakula na sarafu duniani kote ni mambo pia ya kukaa na kutafakari kwa pamoja" alisema Samia.

Aidha aliyataja mabadiliko hayo ni kubadilika kwa muelekeo wa uchumi wa dunia. Alisema ukuaji mkubwa wa uchumi ikiwemo uzalishaji, uwekezaji, biashara, ubunifu na uvumbuzi vimehamia kwenye bara la Asia.

Alisema bara la Asia kwa sasa linazalisha asilimia 40 ya pato la dunia na kuwataka mabalozi hao kujadili jinsi ya kuingia huko ili kuvuna matunda hayo.

Mabadiliko mengine, alisema ni kuongezeka kwa kasi kwa utengamano katika bara la Afrika ikiwamo kupanuka kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuongezeka wanachama kutoka watano hadi saba baada ya kujiunga Sudani Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Rais pia alisema kuanza kutekelezwa kwa itifaki ya soko huru la Afrika na kuibuka kwa mahitaji mapya ya ndani ikiwamo kukua kwa uchumi hasa katika uchumi wa bluu kunahitajika kutafakariwa vizuri na kuwekewa mikakati.

Aidha, aliwataka mabalozi hao kulifanyia kazi suala la kupanuka kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili duniani na mchango wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi na maslahi yao huko waliko.

"Waswahili husema lisilo budi hutendwa, hivyo basi hatuna jinsi zaidi ya kujipanga kukabiliana na mabadiliko haya kwa kuangalia vipaumbele vyetu ikiwamo kufanya mapitio ya sera na kuainisha mabadiliko yaliyotokea duniani,"alisema Rais Samia.

Aliwataka kuongeza uwajibikaji, kuhakikisha wanashirikiana na wadau wote muhimu ili diplomasia kwenda na wakati, ubora na ufanisi. Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, alisema Tanzania imeteuliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Amani la Usalama la Umoja wa Afrika kwa kipindi cha miaka miwili. Alisema hatua hiyo inawezesha kuwa na kauli katika ulinzi na usalama wa taifa na jumuiya ambazo Tanzania ni mwanachama.




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akisimamisha magari ili kuruhusu wanafunzi kuvuka barabara alipowafundisha kuhusu elimu ya usalama barabarani, eneo la Pugu Kajiungeni jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Rais Samia awapa jukumu viongozi dini ulinzi mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewapa jukumu la ulinzi wa mazingira viongozi wa dini, akisema athari za mabadiliko ya tabianchi zinazojitokeza kwa sasa ni matokeo ya uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji uliofanyika kwa miaka mingi.

Akizungumza jana jijini hapa wakati wa Jubilee ya Miaka 50 ya Utume wa Kanisa la Waadventista Wasabato Dodoma, Rais Samia alisema maeneo mengi nchini yamekuwa na misimu ya mvua isiyotabirika na mingine kukumbwa na ukame kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Nitoe wito kwenu na niwaombe viongozi wa dini wote nchini kumwomba Mwenyezi Mungu atunusuru na madhara haya na kutushushia neema ya mvua, lakini wakati tukifanya hivyo tuelimishane na kuhimizana wajibu wetu wa kutunza mazingira pamoja na vyanzo vya maji.

"Adhabu tunayopata leo ni kwa sababu kwa kiasi kikubwa tumeharibu mazingira yetu, tumeenda kuvikera vyanzo vya maji, tumekwenda kuharibu mazingira, hivi karibuni mmekuwa mkituona tukihangaika makundi kwa makundi ya ng'ombe yanahama kundi moja kwenda kufuata maji maeneo mengine.

"Ng'ombe 2,000 au 3,000 wakiingia kwenye mto, ng'ombe mmoja anakunywa lita 45 kwa siku, ng'ombe 3,000 watakunywa lita ngapi? Huo mto utabaki kweli?

Hauwezi kubaki na wakati huu wa kiangazi, kwa sababu hiyo maji hayatiririki yanapochakatwa na kusafishwa kwenda kwa wanadamu.

"Tuliopo mjini tunafurahia sana kupikia mkaa bila kujua mkaa ule unatokana na miti iliyooteshwa miaka kadhaa, imekatwa imechomwa ndipo wewe unapikia, ukiangalia gharama za mkaa mpaka unapokufikia unaweza kusema hakuna nishati rahisi ya kupikia kama mkaa. Miti tunayokata miaka na miaka matokeo yake ndiyo tunayaona leo, vyanzo vya maji vimekauka, unyevu nchini haupo," alitahadharisha.

Alisema kuna upungufu mkubwa wa vyanzo vya maji kutokana na uharibifu huo, hivyo kusababisha uhai kuwa matatani kwa kuharibu mazingira.

Aliwaomba viongozi wa dini kutetea uhifadhi wa mazingira na kujitolea kupanda miti kwa wingi ili kurudisha mazingira yaliyoharibiwa.

"Hatua tuliyofikia kwa sasa tunaadhibiwa kwa kuharibu mazingira, hivyo turudi kupanda miti kwa wingi, kutunza vyanzo vya maji, misitu iwapo kwa wingi, ombi langu kwenu ni kutunza na kusimamia mazingira yetu," alisema.

Rais pia alisema kuwa kupitia maombi ya viongozi wa dini, taifa limeendelea kudumu katika uzalendo na mshikamano, akionya kuwa taifa halitaweza kipiga hatua kimaendeleo kama hakuna mshikamano na amani.

Alioneshwa kuvutiwa na namna kanisa linavyowalea vijana na watoto ili wakue kwenye maadili mema na kumcha Mungu.

"Ninataka niseme nimefurahishwa mno na kwaya mbili zilizoimba hapa, wameimba maudhui ya kizalendo na wamejengwa kizalendo, mnasaidia sana serikali maana bila hivyo magereza yetu yangekuwa yamejaa, vyombo vya ulinzi na usalama vingekuwa na kazi ngumu sana ya kupishanapishana huku panya road, majaji wetu wangekuwa kazi kubwa sana.

"Tunashukuru sana kwa kusaidia malezi, kujenga maadili na kukuza wazalendo wema wa taifa hili. Huu ni wito kwa viongozi wa madhehebu ya dini mbalimbali nchini kuwahimiza watanzania kuzingatia mila na maadili ya kitanzania.

"Ninatambua kanisa hili limekuwa likishirikiana na serikali kwa shughuli mbalimbali za kijamii, hususan afya na elimu ambapo mnaendesha shule za msingi, sekondari, vyuo, pia mmejenga na kuendesha zahanati, ninatambua mchango wenu kwa nyanja mbalimbali za afya na maisha bora," alisema.

Rsis alisisitiza serikali inatambua mchango wao na wa madhehebu yote ya dini nchini katika ujenzi wa taifa na kuomba waendelee kuiombea Tanzania idumu katika misingi ya mshikamano na amani ili kuleta mabadiliko ya kweli na kupiga hatua zaidi katika kujiimarisha kiuchumi. Kuhusu vikwazo mbalimbali, Rais Samia alisema suala la usaili na ufanyaji mitihani siku ya Jumamosi litaangaliwa vizuri.

Kuhusu kufutiwa kodi zinazotozwa kwenye taasisi za elimu za kanisa ili kurahisisha utoaji huduma kwa jamii, uhitaji wa madaktari bingwa kwenye hospitali za kanisa hilo na kanisa kutambuliwa na serikali kutokana na kutokuwapo kwenye mwamvuli wowote wa umoja wa madhehebu ya kikristo, Rais Samia alisema mambo hayo yataangaliwa.

"Pia ninatambua hamjasema deni nililorithi kwa mtangulizi wangu, Hayati Rais John Magufuli ya kusaidia ujenzi wa nyumba ya ibada Chamwino, niseme tu baadhi ya maombi yanaweza kupatiwa majibu kwa haraka na mengine yanahitaji mashauriano ya kina na wenzangu serikalini, niseme maombi yote ninayabeba na tutafanyia kazi na tutawapa mrejesho baada ya mashauriano na wenzangu serikalini," alisema.

Naibu Waziri Wizara ya Katiba na Sheria, Geofrey Pinda alisema serikali haina mlengo wa dini na kusisitiza kuendelea kushirikiana na taasisi za dini katika maeneo yanayowagusa.

Awali akitoa taarifa ya kanisa, Katibu Mkuu wa Jimbo la Kati, Jeremia Izungu alisema usaili wa nafasi za kazi zinazotangazwa na serikali mara nyingi hufanyika siku ya Jumamosi ambayo ni siku ya ibada takatifu, kitendo kinachowanyima haki vijana wa Kisabato kuingia kwenye mchakato wa kupata ajira.

"Baadhi ya vyuo na shule wanafanya mitihani siku ya ibada yaani Jumamosi, pamoja na miongozo mbalimbali kutolewa na serikali bado baadhi wanalazimisha Waadventista Wasabato kufanya mitihani na wanapoacha kufanya mitihani wanapoteza njozi zao za kuendelea na masomo yao ambayo ni haki ya msingi ya kila Mtanzania," alisema.

Aliomba serikali kuwapatia madaktari bingwa kwa ajili ya hospitali za kanisa hilo na kufutiwa kodi inayotozwa kwenye taasisi za elimu za kanisa ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii ya watanzania.

Askofu Mkuu wa Jimbo kuu la Kusini mwa Tanzania, Dk. Godwin Lekundayo alisema kanisa linashirikiana na serikali katika utoaji wa huduma za kijamii, kama afya, elimu, uchangiaji wa damu na malezi ya vijana ili kuwa na wananchi wenye tabia njema na uzalendo.

# 160,000 kukabiliwa uhaba wa chakula

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WATU 166,092 wamebainishwa kuwa watakuwa na upungufu wa chakula wa jumla ya tani 11,211 mkoani Singida kuanzia mwezi Desemba mwaka huu hadi Februari mwakani.

Katibu Tawala Msaidizi - Uchumi na Uzalishaji, Stanslaus Choaji akizungumza katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), alisema katika msimu wa kilimo wa 2021/22 mkoa ulilima hekta 470,000 na kufanikiwa kuvuna tani 649,850 za mazao ya chakula.

Alisema mahitaji ya chakula kwa mwaka mzima kwa wakazi wote wa Mkoa wa Singida wanaokadiriwa kufikia 2,008,058 ni tani 542,175.7, hivyo kiasi hicho kilichovunwa ambacho kinatumika katika mwaka 2022/23 kinaufanya mkoa kuwa na utoshelevu wa chakula ziada ya tani 107,674.

"Takwimu zilizopokewa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaonyesha kuwapo upungufu wa chakula ambao utajitokeza kuanzia mwezi Desemba 2022 hadi Februari 2023," alisema.

Choaji alisema tatizo lililopo kwa sasa ni bei kubwa ya chakula katika masoko ya ndani na nje ya mkoa ambapo upatikanaji wa chakula umekuwa wa shida kwa kaya za familia zenye kipato kidogo.

"Gunia la mshindi lenye ujazo wa kilo 100 ni Sh. 110,000 hadi 118,000, kilo moja ya unga wa sembe ni Sh. 1,700 na unga wa dona ni Sh. 1,600, kilo moja ya mchele ni Sh. 2,500 hadi 3,500 na maharage kilo moja ni Sh. 3,000 hadi Sh. 3,500," alisema.

Choaji alisema ili kukabiliana na tatizo la chakula kuuzwa bei kubwa, mkoa kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa unawasiliana na Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ili walete mahindi yatakayouzwa kwa bei nafuu kulinganishwa na bei zilizopo sokoni.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi tayari imekwishawasiliana na NFRA na imepatiwa tani 100 za mahindi yanayouzwa kwa bei ya Sh. 830 kwa kilo moja. Kuhusu mkakati wa kilimo kwa msimu wa 2022/23, alisema mkoa unatarajia kulima hekta 615,142 na matarajio ya kuvuna tani 1,300,232 za mazao ya chakula.

Alisema kiasi kilicholengwa kitauhakikishia mkoa kuwa na utoshelevu katika suala la usalama wa chakula na upatikanaji wa chakula kwa wananchi wake wote kwa mwaka mzima ambapo mahitaji ni tani 542,175 kwa mwaka.

Choaji alisema kwa mazao ya biashara, mkoa unatarajia kulima hekta 424,647 na kuvuna tani 843,959 ifikapo Juni mwakani.



Msongamano wa magari unaosababishwa na ujenzi unaoendelea katika eneo la njiapanda ya Barabara ya Kilwa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Zitto aliamsha sakata gesi asilia

**Na Romana Mallya**

KIONGOZI wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe ameliibua sakata la gesi asilia ya Mtwara, akitaka serikali iweke wazi mikataba kwa kila hatua ili wananchi waijadili na kufanya uamuzi kadri watakavyoona inawanufaisha.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wanachama na viongozi wa chama hicho katika kikao cha ndani kilichofanyika mjini Lindi.

Zitto alisema: "Uzoefu wa mikataba ya gizani inazalisha hofu. Tunaendelea kusisitiza serikali iweke wazi mikataba ya kila hatua ili wananchi waijadili na kufanya uamuzi kwa kadri watakavyoona inawanufaisha."

Kiongozi huyo pia alisema chama chao kinaona hatua ya kuwahamisha wananchi na kuwapatia fidia tu ili kupisha shughuli za uchimbaji haitoshi.

"Wananchi, vijiji na maeneo inakopatikana gesi wanapaswa kushirikishwa na kupewa sehemu ya umiliki wa shughuli za uchimbaji katika maeneo yao.

"Tunapendekeza Halmashauri ya Lindi kupewa hisa ya asilimia 2.5 kutoka ardhi yao, hii itasaidia kwa wananchi kupata mgawo wa faida ya uwekezaji kila mwaka na kushiriki moja kwa moja kwenye vikao vya uamuzi," Zitto alisema.

Kiongozi huyo aliitaka serikali kuhakikisha ndoto na matumaini waliyopewa wakazi wa kusini na watanzania tangu kugundulika kwa gesi asilia kwenye Pwani ya Bahari ya Hindi, inatimizwa.

"Hofu ya watanzania na kushuka kwa matumaini kuhusu manufaa ya gesi kwa taifa ni kutokana na uzoefu wa uwekezaji wa gesi ya Songosongo na Mnazimmoja kuwa na mchango hafifu kwenye maendeleo na sekta ndogo ya umeme," alisema. Zitto alisema wananchi wametaja kuwapo kwa maandalizi madogo ya uwezeshwaji wa wazawa, umiliki na ushiriki wao.

"Kuna malalamiko ya wananchi waliohamishwa kwenye ardhi zao kucheleweshewa na kupunjwa kwa fidia," alisema.

Zitto alisema ugunduzi wa gesi na kuanza kwa uwekezaji kuliibua ndoto na matumaini ya kuivusha Tanzania kiuchumi na kijamii.

Alisema ipo hofu kuhusu matumaini hayo kwa kile alichokiita usiri wa mikataba, ushirikishwaji mdogo na kufungamanishwa kwa uwekezaji huo na maendeleo ya watu. "Katika hatua za awali, tunasikia malalamiko kutoka kwa wananchi waliohamishwa au wanaopaswa kutoka maeneo yao ya asili ili kupisha uchimbaji na uwekezaji wa gesi, kutolipwa na kucheleweshewa fidia ya ardhi yao," alidai. Zitto alisema yapo makosa aliyoyaita kuwa ni uzembe baada ya wananchi hao kuondolewa kwenye ardhi yao, kutonufaika zaidi na ardhi waliyoitoa na haihesabiwi kama ni uwekezaji kwenye mradi wenyewe.

Pia alisema kuwa watanzania wanatakiwa kuandaliwa kupitia utaratibu wa uwezeshaji wa wazawa kupokea uwekezaji huo ili watoe huduma, kuendesha na kunufaika moja kwa moja.

"Katika kukabiliana na changamoto zinazojitokeza kuelekea uwekezaji mkubwa kwenye gesi asilia, serikali ichukue hatua na kutorudia makosa kutokana na uzoefu wa ndani na nchi jirani," alishauri.

# UVCCM yamjia juu Bashiru, yamtaka kuomba radhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) umemjia juu mbunge wa kuteuliwa, Dk. Bashiru Ali na kumtaka kuomba radhi kutokana na kauli yake aliyoitoa hivi karibuni ya kuonyesha kukerwa na wanaosifia utawala kwa kutumia maneno 'anaupiga mwingi'.

Dk. Bashiru ambaye amewahi kuwa Katibu Mkuu wa CCM, juzi akiwa kwenye mkutano wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA) mkoani Morogoro, alinukuliwa akisema maneno mbalimbali yaliyotafsiriwa na umoja huo kuwa yana ukakasi kwa kuwa yametolewa na aliyekuwa kiongozi wa chama hicho na hakusita kupongeza serikali kwa wakati huo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu Mkuu wa UVCCM, Kenani Kihongosi, alisema: "Amezungumza maneno ambayo si rafiki, si ya kiungwana, yamejaa ukakasi na yamelenga kuchonganisha serikali na wananchi, hasa wakulima.

Kihongosi alisema serikali imeweka utaratibu wa wakulima kununua mbolea kwa bei nafuu, jambo ambalo limegusa maisha yao na uchumi wa nchi.

"Sasa anapotokea kiongozi ambaye alikuwa na dhamana kubwa anatoa maneno yenye ukakasi kwamba viongozi hawapaswi kupongezwa, bali wanapaswa kutolewa matamko ya kuwashinikiza, hii sio sawa, nitoe rai kwa viongozi, tabia hii sio njema.

Alifafanua kuwa Dk. Bashiru ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na anajua kila kilichofanyika kwenye sekta hiyo na namna bajeti ilivyoongezeka katika mwaka huu wa fedha, hivyo anapofikia kutoa kauli hiyo ni jambo la kushangaza.

"Tujikumbushe ndugu Bashiru akiwa kiongozi mara nyingi ametoa pongezi kwa serikali na amekuwa akipongeza kwa kazi nzuri na njema iliyokuwa inafanywa na serikali sasa heshima aliyoitumia kipindi kilichopita, heshima ileile aitumie kwa kipindi hiki kwa sababu serikali bado ni moja na chama bado ni kilekile, wajibu wake ni kuwa na utii kwa mamlaka ambayo ipo madarakani," alisema.

Nipashe ilimtafuta Dk. Bashiru kuzungumzia suala hilo, lakini simu yake iliita pasina kupokewa na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi ili kutoa ufafanuzi, hakujibu.


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AKON ANTON** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 632 BVC – BOXER NYEUSI.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PWA/MLA/RB/399606/2022.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA KANDA YA SUMBAWANGA RUFAA YA MADAI NAMBA 6/2020 (Kutoka Mahakama ya Watoto Mpanda shauri la madai na.4/2022)**

**FABIAN PETER KASHINJE ..........MRUFANI**

**DHIDI YA**

**EDA MANUFRED NDOMBA.......MRUFANIWA**

**WITO WA KUITWA SHAURINI.**

**KWA EDA MANUFRED NDOMBA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA** Shauri tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya SUMBAWANGA mnamo tarehe 22/11/2022 mbele ya Mh. Dustan Beda Ndunguru,JAJI wa Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya SUMBAWANGA kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

**HIVYO BASI** ufike wewe au wakili wako tarehe hiyo **UNAFAHAMISHWA** kuwa shauri linaweza kusikilizwa pasipo wewe kuwepo.

IMETOLEWA kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 18 Mwezi Novemba 2022.



RIPOTI MAALUM

# Punda wa kukodisha walivyogeuka lulu ukame ukiwaandama wanakijiji

## ■Wamiliki waweka masharti idadi ya madumu
## ■Kisima chaokoa ndoa, kuzuia mimba za utotoni

**Na Beatrice Shayo, aliyekuwa**
MPWAPWA

NI majira ya mchana, kijijini Sazima, njiani anaonekana mama mwenye umri wa makamo akiwa amebeba kichwani dumu la lita 20 huku akiwaswaga punda wawili waliobebeshwa madumu mawili kila mmoja.

Mahali hapo penye ushuhuda huo wa Nipashe, ni ndani ya Kata ya Mima umbali wa Km 46 kusini magharibi mwa Mji wa Mpwapwa mkoani Dodoma.

Nipashe inaguswa na kinachojiri na kuamua kupata ufafanuzi kutoka kwa wenyeji, mama huyo wa mtoto mmoja anayejitambulisha kwa jina la Paulina Kimosa, akitamka:

"Mimi ninatokea Kitongoji cha Makutupa (kijiji Sazima), nimekuja kuchota maji hapa (Kitongoji cha Chikola) ninatumia zaidi ya saa mbili kuyafuata, mapambano yake ni kuwahi kufika ili usikutane na foleni.

"Huwa ninaamka saa 11 alfajiri ili kuwahi kuchota maji katika kisima hicho na kurejea nyumbani kwangu majira ya saa nne (asubuhi) na wakati mwingine hadi saa sita mchana."

Mama huyo anayeonekana kuandamwa na uchovu, anabainisha kuwa mwaka huu wamekumbwa na ukame uliosababisha vyanzo vingi vya maji kukauka isipokuwa kisima hicho ambacho sasa kinategemewa na kijiji kizima cha Sazima.

"Maji ya kisima hicho sasa yanategemewa na watu wengi, kuna muda ninakutana na foleni na kukaa hata kwa saa mbili hadi tatu ndipo ninafikiwa na zamu ya kuchota maji.

"Nikichota dumu moja huwa halitoshi matumizi ya nyumbani kwangu, inanilazimu kurudi mara ya pili jioni kufuata maji ili yatosheleze mahitaji.

"Unarudi nyumbani na dumu moja, hapo hapo unataka kufua, unataka kuoga, hujapika, halinitoshi hili dumu moja. Kazi kubwa kwangu kwa sasa ndiyo hii ya kuchota maji, inanilia muda wangu," analalamika.

Kutokana na uhitaji mkubwa wa maji nyumbani kwake, Paulina (50) anasema inamlazimu kukodi punda kwa ajili ya kubeba maji, huku wamiliki wakimpa masharti ya kutozidi madumu mawili kwa kila punda.

"Hawa punda wawili ninalipia Sh. 2,000, (wamiliki wa punda) hawataki uzidishe madumu ya maji, mwisho mawili kwa punda mmoja. Kuna wakati ninakosa hizo fedha za kulipia, ninachokifanya ninachukua mtama kilo nne ninampatia mwenye punda, naye ananipa punda ninakwenda kuchota maji.

"Bila kufanya hivyo, ninajikuta ninatumia muda mwingi kufuata maji na majukumu mengine ninashindwa kuyatekeleza kama kupika kwa wakati na hata shughuli zangu zingine.

"Kuna muda foleni inakuwa kubwa maana hata wenye mifugo nao wanaileta kisimani kupata huduma ya maji, unajikuta unafika nyumbani saa sita mchana, unapochelewa kupata maji, ukishafika nyumbani mume naye anakutuhumu ulikuwa kwenye pombe au kwa wanaume. Hapo unakumbana na kipigo," Paulina anafafanua.

Anawasilisha kilio chao cha muda mrefu, akiomba serikali iwajengee visima vya maji katika kitongoji chao ili kuachana na kutembea umbali mrefu kufuata maji kwenye vitongoji vingine yanakopatikana.



Sera ya Maji inayotumika nchini kwa sasa, inaielekeza serikali ihakikishe wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama ndani ya mita 400 kutoka kwenye makazi yao.

**TIJA YA KISIMA**

Malkia Majaliwa, mwenye makazi karibu na kisima hicho tegemeo, anasimulia namna kilivyoleta ukombozi kijijini Sazima kipindi hiki cha ukame.

Mama huyo wa watoto watano anasema kisima hicho kisingekuwapo, ingewalazimu kwenda kuchota maji umbali wa kilomita saba hadi tisa kama ilivyokuwa awali.

Anabainisha kijiji chao kimekuwa kikikumbwa na ukame mara kadhaa lakini mwaka huu wameona umeongezeka zaidi, wakishuhudia visima vyao vya kienyeji vikikauka.

"Maji hapa yanapatikana kama kawaida licha ya ukame, kuna wakati unakuta foleni ndefu, unasubiri zamu ikifika unachota. Ukame huu haujaathiri kisima hiki, tumepata athari nyingine katika mazao na vitongoji vingine visima vyao vimekauka," anasema.

Malkia anakumbusha kuwa kabla ya kujengewa kisima hicho na serikali, walikuwa wanakumbana na anachokiita mateso wakati wa kusaka maji ikiwamo kukutana na wanyama wakali porini, akiwataka baadhi yao -- fisi na simba.

"Tulikuwa tunakwenda kutafuta maji usiku na watoto mgongoni, tunapanda milima na kuna muda tunaanguka katika vilima, maji yanamwagika na hapo umeyahangaikia kwa zaidi ya saa sita, tulikuwa tunateseka sisi!

"Kwa kweli watoto wangu watano nimejifungua katika mazingira magumu. Ukishakula chakula cha usiku, unaanza safari ya kwenda milimani kusaka maji, hapo kurudi ni kesho yake," Malkia anakumbuka waliyopitia.

Mkazi huyo wa Sazima anaeleza kuwa baadhi ya wanafunzi walipata ujauzito kutokana na vikwazo vilivyokuwapo porini, hivyo kujifungua katika umri mdogo.

Mbali na mimba za utotoni, Malkia anasimulia madhila mengine yaliyowakumba wanawake yakijumuisha vipgo kutoka kwa waume zao na wengine kuachika kutokana na kuchelewa kurejea nyumbani.

"Yaani kipindi hicho tulikuwa tunatembea saa sita kusaka maji, ukifika unakutana na foleni, tunalala kwenye majani ili kusubiria zamu ya kuchota walau ya kupikia, kuoga kwetu hakikuwa kipaumbele.

"Bahati nzuri kwangu ni kwamba mume wangu nilikuwa ninakwenda naye, zile hekaheka aliziona, hiki kisima ni mkombozi wa ndoa za wanawake wenzangu wengi, tuliteseka sana," Malkia anawasilisha.

Ni kauli iliyoungwa mkono na Yunus Fundi, mkazi mwingine wa kijiji hicho anayesema kisima hicho sasa ni kimbilio la watu wengi ingawa mpaka akifikie, inamlazimu kutembea umbali wa kilometa moja kutoka kwenye makazi yake.

"Tunachokiomba maji yasipungue maana ukame umezidi, tunasikia vitongoji vingine vinapata shida na kugombea maji na wanyama. Hii ina maana kwamba maji yakikatika hapa, tutarudi tulikotoka katika mateso ya kufuata maji umbali wa kilomita saba.

"Hayo maji yenyewe tuliyokuwa tunayafuata umbali mrefu, si safi na salama kwa binadamu. Kuna wakati tulikuwa tunawashwa tulipoyaoga," anasema.

**MIKAKATI SERIKALINI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Watumiaji Maji Sazima, John Mataluma anasema kijiji hicho kina vitongoji 10. Kati yake, saba vinatumia maji ya kisima hicho na vingine vitatu vinatumia maji kutoka kwenye visima vya kienyeji.

"Bado tuna changamoto ya upatikanaji wa maji, wananchi wanatembea umbali mrefu kufuata maji, hivyo muda mwingi unapotea katika kutafuta maji na kujikuta shughuli nyingine ya kiuchumi zikidorora.

"Tunamshukuru Mungu licha ya kuwapo ukame na athari zingine za mabadiliko ya tabianchi, kisima hiki kilichojengwa na serikali kinaendelea kutoa maji kwa wingi, hakuna wanaokosa huduma hiyo.

"Kisima chetu kinatoa maji vizuri, watu wengi wanakuja kuchota maji na wengine wanatokea kijiji jirani cha Igoji, wanakuja hapa kuchota maji, mifugo yao pia inakunywa hapa," anasema.

Mwenyekiti huyo anabainisha kisima hicho sasa kinatoa huduma kwa zaidi ya watu 500 kwa siku huku wakiweka utaratibu wa malipo ya Sh. 40 kwa dumu, akisisitiza ni bei elekezi kutoka serikalini kwa visima vinavyotumia pampu ya umeme.

Diwani wa Mima, Bezarery Mnyambwa anakiri kisima hicho kuwa mkombozi kwa wanawake waliokuwa wanautumia usiku kusaka maji badala ya kulala majumbani, hivyo kuhatarisha ndoa zao na hata usalama wao. Meneja wa RUWASA Wilaya ya Mpwapwa, Cyprian Warioba anasema wana mradi wa maji wa muda mrefu katika Kijiji cha Sazima ambao hata hivyo hautoshelezi mahitaji kutokana na wingi wa watu.

Warioba anasema mkakati wao katika bajeti ya mwakani ni kuongeza ukubwa wa tangi na miundombinu ya maji ili kuwawezesha wakazi wa kijiji hicho kupata maji safi na salama.

Hali hiyo inayokinzana na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 - 2025 inayoielekeza serikali kuhakikisha wananchi wanaoishi katika umaskini wanawezeshwa kupata huduma muhimu za kijamii ili kuwafanya waishi katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Juni 15, 2022 Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji ya Maendeleo (UNCDF) walitoa Sh. milioni 343.9 kwa ajili ya kujenga uhimili wa athari za mabadiliko ya tabianchi.

Programu hiyo inatekelezwa katika halmashauri za Chamwino, Mpwapwa na Kondoa mkoani Dodoma na fedha hizo zitatumika kuwawezesha wananchi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususani ujenzi wa miundombinu ya maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani na umwagiliaji.

HABARI KITAIFA

# Daktari aeleza alivyochota damu ya daktari mwenzake

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Angela Mwakibonga, amedai kuwa walichota lita tatu na nusu za damu kwenye kifua cha Dk. Honoratus Mbunda wa zahanati ya Mico aliyepigwa risasi na watu wanaodhaniwa kuwa majambazi.

Mbali na kueleza hayo, Dk Mwakibonga amemshangaa wakili wa utetezi, Mohamed Majaliwa, baada ya kumuuliza kama anawafahamu watu waliompiga risasi Dk. Mbunda.

Dk. Mwakibonga alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Elizabeth Nyembele, wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakati akitoa ushahidi dhidi ya mshtakiwa Julius Mwita anayedaiwa kufanya mauaji hayo.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Dorothy Massawe, Dk. Mwakibonga alidai alifanya uchunguzi wa mwili wa marehemu huku akibainisha kuwa kwa nje aliona nguo zote zikiwa na damu pamoja na majeraha mbele na nyuma.

Alidai kuwa aliufungua mwili kwa ndani ili aangalie vitu vya ndani viko katika hali gani na kukuta maini na figo vimepasuka na kifua kimejaa damu na walipoichota ilikuwa lita tatu na nusu.

Dk. Mwakibonga alidai kuwa kutokana na majeraha aliyokuwa nayo marehemu na uharibifu uliofanyika, chanzo chake kilikuwa kupigwa risasi na kwamba uchunguzi huo ulifanyika saa 24 baada ya kifo kutokea.

Akijibu maswali ya Wakili Majaliwa, Dk. Mwakibonga alidai kuwa: "Mimi kazi yangu ni kufanya 'post-mortem' (uchunguzi). Hayo mambo mengine siyajui kwa sababu hayanihusu kabisa," alidai Dk Mwakibonga huku akionesha kushangaa sana

Ilidaiwa kuwa Novemba 30, 2017 mshitakiwa Julius Mwita akiwa eneo la Kitongoji cha Chakenge, Kata ya Msongola ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, alimuua Dk. Mbunda akiwa katika zahanati ya Mico.

## Bodaboda auawa na kuporwa pikipiki

**Na Mathias Marwa,** MUSOMA

MTU mmoja ambaye hajafahamika kwa jina, ameuawa na watu wanaosadikiwa majambazi katika Kijiji cha Nyabange, Wilaya ya Butiama mkoani Mara.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mara, Loinginus Tibishubwamu, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Novemba 17 mwaka huu wakati mtu huyo akiwa barabarani akiendesha pikipiki.

Kwa mujibu wa Kamanda Tibishubwamu, mtu huyo anayekadiriwa kuwa na umri wa kati ya 30 na 40 alikuwa ni mwendesha pikipiki (bodaboda) katika Manispaa ya Musoma.

Alisema mwili wa kijana huyo umekutwa na majeraha kwenye sehemu mbalimbali, ikiwamo shingoni, kichwani na tumboni.

"Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Mkoa wa Mara mjini Musoma. Jeshi la Polisi linawataka wananchi waliopotelewa ndugu ambaye ni bodaboda tangu tarehe hiyo waende kumtambua hospitalini," alisema.



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi akipata maelezo ya maendeleo ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, kutoka kwa Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kulia), inayojengwa eneo la Lumumba, Wilaya ya Mjini Unguja, jana. **PICHA: IKULU**

# Dk. Mwinyi apongeza utendaji wa mabalozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema serikali inatambua na kuthamini kazi nzuri inayofanywa na mabalozi wa Tanzania wanaoiwakilisha nchi nje ya nchi.

Amesema mabalozi ni taswira ya nchi wanakofanyia kazi na uwakilishi wao ni muhimu katika kujenga ushirikiano kati ya Tanzania na mataifa mingine duniani na hata kujenga uchumi na ustawi wa nchi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mkutano wa mabalozi wa Tanzania uliofanyika Zanzibar.

Aliwataka mabalozi hao kuzielewa sera za ndani na kuzitangaza katika sehemu zao za kazi ili nchi inufaike na fursa zilizopo katika nchi wanazofanyia kazi.

Dk. Mwinyi pia aliwataka mabalozi hao kujenga taswira nzuri ya nchi na kuongeza ubunifu na kuvifahamu vipaumbele vilivyopo kwa ajili ya kuimarisha uchumi na kukaribisha wawekezaji.

Alisema mabalozi ndiyo wawakilishi wa nchi ambao wanatakiwa kuvifahamu vipaumbele vyote ambavyo ni mahitaji mahsusi kwa nchi, hatua ambayo itawasaidia wawekezaji.

Aliitolea Zanzibar ambayo ina Dira ya Maendeleo ya 2020-2050 huku ikitekeleza Ilani ya CCM iliyojikita katika vipaumbele vya uwekezaji wa uchumi wa bluu ambao unahusisha bandari, utalii na uwekezaji katika ujenzi wa bandari kubwa.

Alisema Zanzibar ni visiwa vilivyozungukwa na bahari, hivyo katika sera ya uchumi wa bluu imehimiza na kusisitiza suala la matumizi endelevu ya rasilimali ya bahari kwa ajili ya kulinda viumbe vya baharini.

"Serikali ya Zanzibar iko katika maboresho makubwa ya sera ya uwekezaji ambapo kwa sasa Mamlaka ya Vitega Uchumi na Uwekezaji (ZIPA), mwekezaji anaweza kukamilisha shughuli zake na kupata leseni ya mradi katika kipindi cha saa 24, hivyo ni vyema kutuletea wawekezaji kwa wingi," aliagiza.

Akizungumzia sekta ya utalii, Dk. Mwinyi alisema serikali iko katika mikakati ya kuboresha huduma muhimu ikiwamo ujenzi wa Uwanja wa Ndege Pemba kwa ajili ya kuongeza idadi ya watalii.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Stegomena Taxi alisema wamejipanga kutekeleza maagizo yote wanayopewa na viongozi wakuu wa nchi ili Tanzania inapiga hatua katika sera yake ya diplomasia ya mambo ya nje ambayo imejikita katika uchumi na biashara.

Aliwataka mabalozi kufanya kazi kwa maslahi ya pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huku wakifahamu wizara yake ni taasisi ya Muungano.

Mkuu wa Mabalozi hao, Balozi Dk. Asha-Rose Migiro, alisema wamefurahia kupata fursa muhimu ya kuzungumza na watendaji wa Serikali ya Zanzibar ambao waliobainisha fursa zinazopatikana pamoja na mahitaji ambayo ni vipaumbele.

Alisema wamepata fursa ya kubadilishana mawazo na wadau wa biashara, utalii na uwekezaji ambapo wizara na taasisi za serikali zilishiriki.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hoja za CTI kuhusu vikwazo vya biashara zishughulikiwe

JUZI kulikuwa na hafla ya utoaji Tuzo za Rais kwa Mzalishaji Bora kwa mwaka 2021 ambazo zilifanyika Dar es Salaam huku kampuni ya vinywaji baridi ya bonite inayomilikiwa na kundi la kampuni za IPP, iliibuka mshindi katika kundi la wazalishaji wa vinywaji baridi.

Mbali na kampuni hiyo inayotengeneza soda jamii ya Coca Cola na maji ya Kilimanjaro, Kampuni ya Saruji Tanga inayozalisha simenti aina ya Simba iliibuka mshindi wa jumla, ikifuatiwa na Kilimanjaro Cable na Ando roofing zilizoshika nafasi ya pili na ya tatu.

Katika tuzo hizo ambazo ziliandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), wafanyabiashara na wawekezaji walimweleza Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliyekuwa mgeni rasmi kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan kero mbalimbali ambazo zinakwamisha maendeleo ya sekta binafsi katika ufanyaji biashara, hivyo kushindwa kuchangia pato la taifa na uchumi kwa ujumla.

Miongoni mwa kero zilizowasilishwa na wafanyabiashara hao ni kukithiri kwa bidhaa za magendo sokoni, tozo za stempu za kielektroniki na msongamano wa mizigo bandarini hali inayosababisha kuwaongezea gharama na hata kukwama kufanya shughuli zao kwa ufasaha.

Kutokana na kero hizo, Dk. Mpango aliahidi kuwa serikali itazifanyia kazi na kuzipatia ufumbuzi ili kutokukwamisha maendeleo ya viwanda huku akiziagiza taasisi zinazohusika, vikiwamo vyombo vya dola, kuchukua hatua mara moja.

Kuhusu kuwapo kwa bidhaa za magendo, alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, ambaye eneo lake ni kinara wa bidhaa hizo kuchukua hatua mara moja na kukomesha biashara hiyo ambayo ni kikwazo kwa bidhaa halali ambazo zinatengenezwa katika viwanda vya ndani.

Licha ya kuwapo kwa bidhaa za magendo, Dk. Mpango alieleza kwa kina suala la bidhaa ghafi kuuzwa nje ya nchi badala ya kutumika kuzalisha bidhaa mbalimbali katika viwanda vya ndani, hatua ambayo inasababisha vijana wengi wa Kitanzania kukosa ajira.

Kuhusu tozo za stempu za kielektroniki hasa kwa bidhaa za ushuru, ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wawekezaji na wafanyabiashara kwa muda mrefu kuwa ni kikwazo, Dk. Mpango aliwahakikishia wanachama wa CTI kuwa serikali inalifanyia kazi na taasisi husika na serikali itawashirikisha wadau na suluhu itapatikana hivi karibuni. Licha ya kuahidi kufanyia kazi, alisema tozo hizo zitatolewa kwa gharama ndogo.


Kadhalika alisema msongamano wa mizigo bandarini unafanyiwa kazi huku akiiagiza Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), kulifanyia kazi ndani ya wiki mbili na kuwasilisha taarifa kwa Waziri Mkuu ili kujua tatizo ni nini na hatimaye hatua kuchukuliwa.

Hatua ya serikali ya kusikiliza hoja za wafanyabiashara hasa wenye viwanda ni ya kupongezwa kwa sababu inaonyesha kwamba imedhamiria kuiondolea vikwazo sekta binafsi ili ishiriki kikamilifu karika maendeleo ya uchumi wa nchi.

Kama alivyoagiza makamu wa Rais, ni vyema taasisi zinazohusika na masuala yaliyoelezwa kuwa ni kero kwa wafanyabiashara zikachukua hatua mara moja kutekeleza masuala hayo ili kuondoa vikwazo vya maendeleo ya viwanda, biashara na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mashine hizi zinaweza kunyoosha madereva wa bodaboda

Na Sabato Kasika

**MASHINE** za kielektroniki zimefungwa maeneo mbalimbali ya barabara jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kuwabaini madereva magari wanaochati na kuongea na simu wakiendesha, ili kudhibiti ajali zinazotokana na uzembe.

Inaelezwa kuwa teknolojia hiyo mpya nchini itakuwa na uwezo wa kurekodi na kupiga picha magari zaidi ya 10 barabarani kwa wakati mmoja, lakini pia na kumpiga picha dereva anayeongea na simu au kuchati wakati anaendesha gari.

Kwamba mfumo huo utachukua makosa yote yanayofanywa na madereva magari, bajaji na hata bodadoda, ukirekodi magari 2,000 kwa saa moja, hasa kwenye barabara korofi ambako ajali zinatokea kwa wingi.

Ninaamini kwamba, iwapo mashine hizo zitaanza kufanya kazi, ni wazi wengi wa madereva watakaobanwa, ni madereva wa bodaboda, ambao wamekuwa mstari wa mbele kuvunja sheria ya usalama barabara.

Limekuwa kama jambo la kawaida baadhi ya madereva hao kutoheshimu sheria, hasa kwenye makutano ya barabara, wakikuta taa za kuongozaa vyombo vya moto hazijaruhusu, wao hulazimisha kupita.

Katika mazingira hayo, wamekuwa wakisababisha ajali zinazoweza kuzuilikia kama wangesubiri taa ziwaruhusu, lakini siku zote wao wana haraka zinazosababisha ajali hata zile zinazozuilika. Matokeo yake huwa wanajikuta wakijisababishia ulemavu wa kudumu kupoteza maisha kutokana na ajali, ambazo chanzo chake ni wao, ambapo hata abiria wao huathirika pamoja na waenda kwa miguu.

Kwa mtazamo wangu ni kwamba, kufungwa kwa mashine hizo kunaweza kuwa na mchango mkubwa wa kusaidia kuwanyoosha madereva hao ambao wamekuwa ni wakaidi kufuata sheria ya usalama barabarani.

Ikumbukwe kuwa hata mtindo wa kupita kwenye barabara za mabasi ya mwendokasi, Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli (hayati), aliwahi kuwakemea na kuwataka wasizitumie.

Hata hivyo, hawakumsikia, lakini pia hivi karibuni, Jeshi la Polisi lilitaja orodha za vyombo vya moto vinavyotakiwa kupita kwenye barabara hizo kwa dharura, bodaboda hazikutajwa katika orodha hiyo.

Lakini madereva wake wanaendelea kuzitumia bila woga kana kwamba hakuna katazo, kitendo ambacho ninaamini kwamba ujio wa mashine hizo za kuwanasa, unaweka hitimisho la madereva wa bodaboda kutofuata sheria.

Kwa kuwa wamekuwa wakitaka kutii sheria kwa shuruti, ninaamini mashine hizo zitawashurutisha, na inawezekana zikawa chanzo muhimu cha kupunguza ajali za barabarani hasa zinazotokana na uzembe wa madereva.

Jambo ambalo ninadhani ni muhimu lizingatiwe, ni kulinda mashine hizo ili ziweze kuleta matokeo chanya zaidi, kwani inawezekana baadhi ya wale wanaobanwa, wakazifanyia hujuma ili waendelee kufanya mambo yao.

Hivyo, ufuatiliaji wa karibu kujua kama zinaendelea kufanya kazi vizuri ni wa muhimu, ili wasijitokeze wasiotaka kufuata ya usalama barabarani na kuzirushia mawe kwa lengo la kutaka kuziharibu.

Pamoja na hayo, ingekuwa ni vyema kama dereva hana mafunzo ya udereva au leseni, asiruhusiwe kuendesha chombo cha moto, kwani njia hiyo inaweza kuliokoa taifa na janga la ajali za bodaboda.

Inaelezwa kuwa asilimia 76.14 ya tabia za kibinadamu ni mojawapo ya vyanzo vikuu vinnne ambavyo vinasababisha ajali za barabarani na kupoteza maisha au kupata majeraha ikiwamo kupoteza mali.

Hiyo ni kwa mujibu wa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Tanga, Leopord Fungu, wakati warsha ya utoaji wa taarifa pamoja na kupata maoni kutoka kwa wadau wa usalama barabarani hivi karibuni.

Kamanda huyo anakemea madereva kuacha kuendesha vyombo vya moto bila kuwa na mafunzo ya usalama barabarani na kuwataka waache njia ya mkato na kwamba wakiacha mtindo huo watasaidia kupunguza ajali.

Kimsingi, huo ndio ukweli mtupu, kwani dereva aliyesomea kazi hiyo, hawezi kusababisha ajali za kizembe kama hizo ambazo madereva bodaboda huwa ni chanzo, hasa kupenda kujipenyeza na kupita kwenye hatari.

Wakati huu ambao zimefungwa mashine ya kuwanasa, ninadhani hata wao wenyewe hawana budi kujiongeza, kwa kuacha mazoea badala yake wawapo barabarani, wazingatie sheria kwa ajili ya usalama wao na wa wengine.

# Tanzania yapiga hatua ubora huduma ya choo

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WIZARA ya Afya imesema kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita vyoo bora katika ngazi ya kaya vimeongezeka kutoka asilimia 19.5 kwa mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 72.6 mwaka huu.

Pia imesema kaya zisizokuwa na vyoo kabisa zimepungua kutoka asilimia 20.5 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 1.4 mwaka huu, huku ikibainisha mtu mmoja ambaye hana choo hupoteza takriban saa 58 kwa mwaka kutafuta mahali pa kujisitiri.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. Seif Shekalaghe alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye kilele cha wiki ya usafi na maadhimisho ya siku ya matumizi ya choo duniani.

Pia alisema ujenzi wa vyoo bora pamoja na kuwapo huduma za maji safi na salama umeongezeka katika taasisi zikiwamo shule za msingi na vituo vya kutolea huduma za afya.

"Ndani ya kipindi cha miaka mitatu iliyopita takriban shule za msingi 2,500 zimejengewa vyoo bora, vituo vya kutolea huduma za afya vipatavyo 1,500 vimeboreshewa huduma ya maji, vyoo na sehemu za kunawa mikono," alisema.

Alibainisha kuwa ufuatiliaji uliofanywa na wizara hiyo kwa mwaka huu unaonyesha katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, zaidi ya vituo vya njiani 280 vyenye vyoo bora vimejengwa na serikali na sekta binafsi, hali iliyopunguza abiria kujisaidia ovyo safarini.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Afya, Mazingira wa Wizara ya Afya, Anyitike Mwakitalima alisema mtu mmoja ambaye hana choo hupoteza takriban saa 58 kwa mwaka kutafuta mahali pa kujisitiri, akifafanua ni muda mwingi kwa nchi inayotaka kupiga hatua kiuchumi.

Alisema kuwapo huduma ya maji, vyoo bora na sehemu za kunawa mikono kumethibitika kuchangia kupungua kwa vifo vya kinamama wakati wa kujifungua kwa kati ya asilimia 17 hadi 25.

"Imethibitika kwamba ukosefu wa huduma hizi husababisha hadi asilimia 45 ya vifo vya watoto wachanga," alisema.

Mwakitalima alisema shule zenye huduma bora za maji na vyoo zimethibitika kuwa na mahudhurio mazuri kwa watoto wote kulinganishwa na zenye huduma duni.

Alisema serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 104 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usafi na huduma za maji kwenye shule na vituo vya afya.

"Kiasi hiki kinatumika kwenye shule za msingi 1,500 na zaidi ya vituo vya huduma za afya 2,500. Aidha, serikali imeandaa fedha kupitia mradi wa BOOST chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia ambao utawezesha ujenzi wa miundombinu bora ya usafi kwa shule zaidi ya 6,000 ifikapo mwaka 2025," alisema.

Mwaka 2025 ni ukomo wa upimaji wa utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Pia ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Junin 1999-2025 inayolenga kupunguza walau nusu ya wananchi wanaoishi katika umaskini na kuwafanya waishi katika uchumi wa kati kufikia mwaka 2025.




Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akijadiliana jambo na wadau baada ya kuzindua duka la vifaa vya kielektroniki la Gadget Mega Store, eneo la Seacliff Masaki mkoani Dar es Salaam juzi. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa Duka hilo, Zeifa Hamid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kamishna Elimu aona fursa lugha ya Kichina

**Na Halfani Chusi**

KAMISHNA Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Lyambwene Mtahabwa amewataka wanafunzi nchini kuchangamkia kujifunza lugha ya Kichina ili wapate nafasi ya kunufaika na fursa nyingi kupitia lugha hiyo.

Dk. Mtahabwa alitoa rai hiyo juzi wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa walimu na wanafunzi waliohitimu lugha hiyo iliyofanyika Ubalozi wa China nchini.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wanafunzi kujifunza lugha hiyo kutokana na uhusiano wa karibu uliopo kati ya China na Tanzania, nchi hizo zinashirikiana katika mambo mengi ikiwamo masuala ya biashara. "China na Tanzania ni nchi ambazo zina uhusiano mkubwa hasa kibiashara kwa miaka mingi, zimekuwa zikishirikiana kwenye maafa mbalimbali pindi yanapojitokeza.

"Kwa hiyo, watanzania wengi wakijua Kichina, itawasaidia hata pale watakapotaka kujiingiza kwenye biashara kwa sababu tayari lugha watakuwa wanaijua.

"Lugha hii inafundishwa katika vyuo mbalimbali nchini, hivyo ni wakati wa kuchangamkia fursa hii, hata mimi ninatamani kujifunza lugha hii kwa sababu nimeona wanaohitimu leo namna wanavyoongea vizuri Kichina," alisema. Aliwataka wanafunzi wanaotaka kujifunza lugha hiyo kupuuza dhana inayojengwa kuwa lugha hiyo ni ngumu.

"Kuna maneno huko mitaani mara oooh lugha ya Kichina ni ngumu, mbona hawa wameweza? Hayo ni maneno ya wakatisha tamaa, yapuuzeni. Ukijua Kichina vizuri, unajiweka katika soko la ajira, unaweza kuajiriwa hata na wachina wenyewe," alisisitiza.

Balozi wa China nchini, Chen Mingjian alisema hiyo ni mara ta tatu kushiriki utoaji tuzo tangu alipowasili nchini na ni mara ya tatu kwa ubalozi wao kufanya sherehe hiyo.

"Ninapenda kuishukuru Wizara ya Elimu, Sayani na Teknolojia na shule zinazotoa msaada wa wanafunzi kujifunza lugha ya Kichina, ni matuamaini yangu kuwa wanafunzi wengi watajifunza Kichina na kupenda utamaduni wetu.

"Jambo zuri ni kwamba kwa mwaka 2021, jumla ya wanafunzi 123 walishinda tuzo ya Balozi wa China na mwaka huu wanafunzi 132 wameshinda tuzo hiyo, hii inaonyesha ni kwa namna gani nchi hii inaunga mkono suala la wanafunzi kujifunza lugha ya Kichina.

"Leo walimu na wanafunzi watatunukiwa tuzo ya Balozi wa China kwa kutambua mchango wao katika kuhakikisha watanzania wengi wanaijua lugha hii vizuri na kuendelea kuunadi urafiki wa China na Tanzania," alipongeza.

# Serikali yatoa angalizo la matumizi nembo ya taifa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

OFISI YA Mpigachapa Mkuu wa Serikali imesema watu wanaotumia nembo ya taifa kujinufaisha katika biashara zao, wanatenda kosa kwa mujibu wa sheria na wakibainika wanaweza kutumikia kifungo cha miaka miwili gerezani au kulipa faini.

Mpigachapa Mkuu wa Serikali, George Lugome aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari mjini hapa kuhusu matumizi ya alama za taifa.

"Yule anayetumia nembo ya taifa eneo lake la biashara maana yake ametenda kosa na Sheria ya Alama za Taifa imeweka wazi anayefanya hivyo anapaswa kuchukuliwa hatua," alionya.

Lugome ambaye alikuwa akijibu maswali ya wanahabari waliotaka kujua mfano watu wanaotengeneza kalenda na kuweka nembo za taifa kama sheria inawaruhusu, alisema hilo ni kosa na wakibainika wanaweza kufungwa jela miaka miwili na faini au vyote viwili kwa pamoja.

"Kuna watu wanachukua nembo ya taifa kwenye mtandao ambazo wamezitengeneza bila kufuata vigezo ambavyo sheria ya alama za taifa inasema na sheria inasema anayetumia alama za taifa isivyo sahihi anafungwa jela miaka miwili au faini," alisema.

Alisema Ofisi ya Mpigachapa Mkuu ndiyo yenye jukumu la uchapaji wa nyaraka zote za serikali lakini pia inasimamia alama za taifa kama nembo ya taifa, bendera na wimbo wa taifa. Lugome ambaye yupo mkoani Singida kwa ajili ya kushiriki mafunzo kuhusu itifaki ya viongozi wa kitaifa yanayofanyika mjini Singida, alisema alama za taifa zinakwenda sambamba na suala la itifaki kwa kuwa kwenye itifaki ndiko alama za taifa zinatumika.

Aliongeza kuwa ofisi yake kabla ya kuanza kuwachukulia hatua watu wanaotumia ovyo alama za taifa, imeanza kutoa elimu. "Hivi sasa kuna changamoto alama za taifa mfano nembo ya taifa inatumika isivyo sahihi, na pia unaweza kukuta bendera ya taifa inashushwa lakini watu wanatembea hawajali, yote hayo tutaanza kuwakumbusha kwenye elimu ya uraia na mitaani," alisema.

Kuhusu suala la kuvuja kwa nyaraka za serikali, alisema limekuwa likijitokeza sana na hii inatokana na kutokufuata utaratibu kwa kwenda kuchapa nyaraka katika sehemu ambazo haziruhusiwi.

"Unakuta ninakwenda kuchapa nyaraka za serikali sehemu ambayo hairuhusiwi na huo ndio unakuwa mwanzo wa kuvuja kwa nyaraka ya serikali," alisema.

Lugome alisema nyaraka za serikali zina alama za kiusalama na serikali inaendelea kuimarisha kwenye eneo la usalama wa nyaraka za serikali.

# MATUKIO KATIKA PICHA



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza wakati akifungua mkutano wa viongozi mbalimbali pamoja na mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi za nje, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi (watatu kushoto), akikata utepe kuzindua rasmi Tawi la benki hiyo katika Jengo la makao makuu ya TPA, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Wengine ni Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa TCB, Gloria Mutta (kushoto), Mkurugenzi wa Masoko, Deo Kwiyuka, Meneja wa tawi hilo, Anastela Kabudi, pamoja na maofisa wengine wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Baadhi ya wanafunzi kutoka shule mbalimbali za msingi, Kata ya Makumbusho, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, wakinyanyua mabango yenye ujumbe wa kuhamasisha vita dhidi ya rushwa ya ngono, kwenye kampeni za Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (katikati), ambaye alikuwa Msimamizi wa Uchaguzi wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Mbeya, akitangaza matokeo ya uchaguzi huo mapema wiki hii, ambapo mgombea, Yasin Ngonyani alichaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa umoja huo mkoa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ng'wilabuzu Ludigija (katikati), akizungumza katika uzinduzi wa kinga tiba ya magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, mabusha na matende, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Rashid Mfaume na Ofisa Mpango wa Taifa wa kudhibiti Magonjwa yaliokuwa hayapewi kipaumbele wa Wizara ya Afya, Oscar Kaitaba. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# MAISHA

NOVEMBA 20, 2022
Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

## Tengeneza Ice Cream nyumbani



Hizi ndizo sababu za kutokea nyufa kwenye nyumba

**MAISHA NI NYUMBA** Ukurasa 15




## KATUNIKA


Ukurasa 16



# NYWELE NYEUSI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



NG'O M B E
NYANI
NGURUWE
KUKU


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | J | A | Z | W | A |
| | A | | | A | |
| A | M | A | | K | |
| | B | | D | A | U |
| | I | | | T | |
| T | A | M | B | I | |

## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
TOA, LIA, TAMBO, SHAKA, KOKOTO, SHINDA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

**Alichokifanya daktari**

WATOTO hawa walipotoka darasani walianza kujadiliana juu ya somo la uraia.

Juma: Eti sisi Watanzania hatuna vazi la taifa?

John: Mwalimu kasema ndio tupo katika mchakato wa kulitafuta

Juma: Sasa huo mchakato unakuwaje, yaani linachakatwa muda wote huo?

John: Yaani lipo kwenye utaratibu wa kulitafuta.

Juma: Kwa nini utaratibu huo usikamilike mpaka tunalikosa hilo vazi?

John: Kama una maswali zaidi kamuulize mwalimu, mimi pia nimefundishwa.

**Swali**

Asili ya lugha ya kiswahili imetokea wapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unalazimishwa ndoa na mwanamume usiyemjua!

KARIBU tena msomaji wangu tudadavue yaliyojificha katika maisha yetu ya kila siku. Wakati mwingine tunayaona ya kawaida kumbe yana chanzo tusichokijua na ndio maana tunaishi maisha magumu hivi leo.

Wiki iliyopita nilieleza kijana mmoja anayetamani kuwajua ndugu zake lakini baba yake alimficha kwani alimzaa nje ya ndoa. Bado anahangaika lakini chanzo ni baba yake ambaye hakumtambulisha kwenye ukoo kabla ya kufariki.

Wazazi wengi wamekuwa chanzo cha matatizo ya watoto wao. Kama walijenga msingi mbovu usiokuwa na ukweli na uwazi, matokeo yake ndio hayo yanaleta sintofahamu kwa watoto baadaye.

Wiki iliyopita niliahidi kuwaletea mifano ya vijana wanaokutana na kuzama kwenye mahusiano, kumbe ni ndugu. Mada hii bado naifanyia kazi nitakuletea wiki ijayo ikikamilika.

Leo nataka nikujuze baadhi ya wazazi wanaolazimisha mahusiano kwa watu wanaowataka wao. Yaani wanamchangulia kijana mke au binti anachaguliwa mume wa kuoana naye. Mfumo huu ulifanya kazi zamani lakini kizazi hiki ni shida!

Hata hivyo, ukitizama kwa undani, zipo roho zinazotesa vijana wengi walio katika harakati za mahusiano. Moja ya 'roho mtego' inayowapumbaza sana vijana ni roho ya ujinga.

Ujinga ni kutokujifunza. Ni kutokuwa na maarifa, kutojifunza mambo mapya. Mtu mmoja akasema, "usipoutawala ujinga, utakutawala wewe na usipoushinda, utakushinda wewe. Wengi wameangamizwa kwa kutokuwa na maarifa!

Wako vijana wengi wa kike na kiume ambao pamoja na shauku yao ya kutaka kuoa au kuolewa na mtu sahihi, wamejikuta wakiingia mkenge kwa kuwa na wenza wasiojuana.

Yaani wanaungana pamoja kabla ya kujua asili au chimbuko la mwenzake. Wengine kwa kulazimishwa na wazazi au kwa kulazimisha wao wenyewe pasipo kushirikisha watu muhimu. Na zaidi ya yote walimweka Mungu kando!

Hebu sikia shuhuda hii. Binti mmoja aliishi na dada yake. Lakini dada akamlengesha kwa mwanaume muuza duka ili aweze kupata mahitaji ya nyumbani. Akamtambulisha dukani.

Taratibu binti akaanza kuzoeana na muuza duka, akichukua bidhaa tu na kuondoka. Siku moja muuza duka akapima sukari na kumwambia binti aingie dukani achukue, kumbe ilikuwa ni mtego. Alipoingia tu akamshika kwa kutumia nguvu za ziada kumdhibiti.

Kutoka pale binti alilia na kumweleza dada kilichompata, naye akamwambia atafuatilia. Kumbe dada alijua mpango ule. Baada ya muda binti akashika ujauzito na dada akamkabidhi kwa yule muuza duka amtunze. Binti hakumtaka yule bwana kwani alimzidi sana umri, lakini angefanyaje?

Binti mwingine akanitumia ujumbe simu ya kiganjani: "Nilipokuwa binti umri miaka 18, Januari mwaka 2016 nilifungishwa ndoa na shangazi yangu bila mimi kumjua mume alivyo! Niliogopa radhi ya wazazi upande wa baba maana baba mwenyewe alimpenda. Nikaletwa Dar nikitokea Lindi.

Ndoa ikawa ngumu kwangu na cha kuumiza zaidi dada yangu aliugua hadi kufariki. Mume huyu hakuniruhusu japo kwenda kumuuguza dada hadi kufariki. Hali haikuwa nzuri kwenye ndoa yangu na mume alinizidi sana umri.

Novemba 2016, akanifukuza na nikidai talaka hataki kutoa. Hadi mwaka ukaisha hataki kutoa. Nikaenda Baraza la Usuluhishi ikashindikana. Wapo waliojitokeza kunisaidia ili niwe huru lakini wapi!

Yule bwana akadai nimlipe sh.360,000 wakati alinioa kwa Sh. 150,000 na pesa yenyewe alipewa na shangazi, naye shangazi alizitoa na kumpa yule aliyenioa ili anunue vitu vya ndani.

Yaani mahari badala ya kupewa mimi akapewa aliyenioa. Sina hela, yupo anayenipenda, lakini talaka sijapewa, nifanyeje?

Mpenzi msomaji, umesikia aliyopitia binti huyu. Ni mume wa kulazimishwa kwani haikuwa chaguo lake.

Ndipo ninapowauliza vijana na mabinti, Je, huyo uliye naye unatamani kuoa au kuolewa naye unamjua? Umechunguza asili yake?

Vijana wengi wanakurupuka kwa kudhani kuoa ni fasheni. Hapana.

Ndoa ni muunganiko kati ya mwanaume na mwanamke kuishi kama mke na mume muda wa maisha yao yote. Pia ndoa ni agano/mkataba wenye kiapo mwanaume na mwanamke kuishi pamoja kimaisha.

Zingatia haya kabla ya kuingia kwenye ndoa. Kwanza mshirikishe Mungu muulize kama ni chaguo sahihi. Mungu ndiye aliyempa Adamu mke (Mwanzo 2:21-22) Pili, dadisi asili ya unayemtaka. Pia jitafakari upo tayari kutunza familia?

**Hadi wiki ijayo. Una maoni au kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tutunze mazingira kwa nguvu zote kuepuka kuangamia

TATIZO kubwa linaloikabili dunia, Tanzania ikiwamo, ni kasi ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamesababisha kukosa mvua za kutosha, ukame, mafuriko na madhara mengine yanayotishia uhai wa watu, hali tunayoiona sasa.

Mabadiliko ya tabia nchi hayasababishwi na eneo fulani pekee bali mchango wa dunia kwa ujumla, nchi za Afrika zikichangia hewa ukaa chini ya asilimia nne huku nchi zilizoendelea zikichangia kwa kiasi kikubwa.

Kwa sasa, hali ya upatikanaji wa maji ni ngumu sana hususan Dar es Salaam, imefikia yanauzwa Sh.1,000 kwa dumu la lita 20 hali inayoongeza ugumu wa maisha.

Aidha, hali hii ni kutokana na kutegemea mvua kama chanzo cha kupata maji, kwa sababu yanachukuliwa kwenye mito na kuna visima vichache.

Mathalani, kwa Tanzania mtu mmoja anachangia gesi ukaa kwa asilimia 0.22 kwa mwaka, huku China na Marekani akichangia asilimia 26 kwa kipindi hicho hicho, kutokana na shughuli za viwanda na nyinginezo ndiyo maana nchi hizo zinatoa fedha za kusaidia kukabili kwa nchi zilizotunza mazingira.

Hadi sasa hakuna mpango kwa nchi hizo kupunguza viwanda, ndiyo kwanza vinaongezeka na ziko tayari kuendelea kutoa fedha kwa nchi zinazochangia kupunguza hewa ukaa kwa kutunza mazingira.

Kwa sasa kila eneo linakabiliwa na ukame huku maji ambayo ni muhimu kwa kila kiumbe yakiendelea kupungua, migogoro baina ya binadamu na binadamu; wanyama na binadamu inaongezeka kwa sababu raslimali hiyo inapotea baadhi ya maeneo.

Ukisafiri kwa anga utaona hali ilivyo ardhini, lakini kasi ya kupaa kwa bei ya nafaka kulikochagizwa na kupaa kwa bei ya mafuta ni udhihirisho kwamba ukame ni tishio, pia unaona mito na maeneo mengine yalivyokauka.

Hivi karibuni, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilieleza mwelekeo wa mvua kuwa si wa kuridhisha, wakulima wameshauriwa aina za mazao ya kulima ambayo ni ya muda mfupi na yenye kuhimili ukame.

Hadi sasa tunaona uhaba wa nafaka huku ikizidi kupanda bei, ongezeko la migogoro baina ya binadamu na wanyamapori ambao wanatoka maeneo yaliyohifadhiwa kwenda kutafuta malisho, huku binadamu nao wakivamia maeneo ya hifadhi kupata mahitaji ya Wanyama wafugwao.

Jitihada nyingi zimefanyika ikiwamo kuhamasisha wananchi kutunza mazingira, kupanda miti kwa wingi na kuachana na matumizi ya nishati ya kuni, ingawa bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa kuwa mkaa unatumika zaidi kutokana na kupaa kwa bei ya gesi.

Hali ya upatikanaji wa chakula ni ngumu sana kwa sasa, nafaka zimepanda bei hali ya maisha inakuwa ngumu kutokana na visababishi vingine kama kupanda kwa bei ya mafuta na COVID-19.

Mabadiliko ya tabia nchi si jambo la kulichukulia rahisi, hivyo lazima nchi iendeleze mikakati yake ya kusaidia wananchi wake kuishi na hali hiyo ambayo haiwezi kuisha leo wala kesho kutokana na kasi ya ukuaji wa maendeleo.

Lazima jamii yetu iendelee kuelimishwa namna ya kutumia fursa katikati ya matatizo, mathalani kwa sasa kuna biashara ya hewa ukaa kwa wananchi waliotunza misitu ya asili, misitu ya kupanda na binafsi ambayo wanauza duniani kwa nchi zilizoharibu au zinazoharibu mazingira.

Misitu hiyo inasaidia kupunguza hewa ukaa kwenye anga na kukabili hali iliyopo sasa ya vipindi vya mvua kutoeleweka, ukame wa muda mrefu, joto na baridi kali kiasi cha kuathiri binadamu na viumbe wengine kama tunavyoona sasa maeneo mengi yana joto kali hadi misitu inawaka yenyewe na kwingine baridi sana.

Kwa sasa usalama wa chakula uko hatarini kwa kiasi kikubwa, kwamba wananchi hawana uhakika wa mlo kamili kutokana na kwamba hawana uhakika wa chakula chenyewe ili waendelee kuwa hai.

Hivyo,kupambana na mabadiliko ya tabia nchi ni lazima kwa kila mmoja lakini wananchi kutumia mbinu zao na za jumla kukabili hali hii, ili dunia iwe salama kwa kila mmoja anayestahili kuifurahia.

Kwa sasa tunasikia migogoro baina ya wanyama na binadamu inashamiri, wanyama wanatoka kwenye maeneo yao ya asili kutafuta malisho na binadamu anapeleka mifugo maeneo yaliyohifadhiwa kutafuta malisho,hii inafanya maisha yasiwe na amani kwenye maeneo mengi.

Mabadiliko ya tabia nchi ni tishio lazima tuwe na mbinu zinazotekelezeka, kubuni namna ya kuendelea kupata maji ya mahitaji ya nyumbani na kilimo cha umwagiliaji kwa sababu cha mvua hakijaonyesha manufaa chanya.

# HARUSI











Ilikuwa Novemba 5, mwaka huu, ndani ya Kanisa Katoliki Parokia ya Mt. Maria iliyoko Kimara, wakati Dk. Honest Kessy na Dk. Josephine Komba walipokula kiapo cha ndoa na baadaye kuandaliwa tafrija fupi iliyofanyika ukumbi wa Tanzanite Kimara jijini Dar es Salaam.





# MITINDO

## VAA KIOFISI ZAIDI



UNAPOFIKIRIA kwenda ofisini ni muhimu kuwaza unavaa nini,hii ni kwa sababu unataka kuonekana nadhifu zaidi.

Moja ya njia ambazo unaweza kuamua nini uvae unapokwenda ofisini ni lazima kufuata taratibu za uvaaji.

Njia hii ni rahisi ukiwa unafanya kazi za kiofisi na ofisi ambayo inakuhitaji kuvaa nguo nadhifu.

Mashati

Ofisi nyingi chaguo lao la kwanza katika mavazi ni mashati, kwa sababu vazi hili linampa mtu mwonekano sahihi na wenye kuvutia.

Pia vazi hili linapendekezwa kutokana na kuwa na aina nyingi ya mitindo, rangi zenye kuakisi utendaji kazi wa ofisi.

**Suruali**

Unatakiwa kuchagua suruali kama vazi rasmi, hii ni kwa sababu suruali inaonekana nadhifu na mara nyingi huendana na koti la suti inayolingana.

Suruali pia zina rangi mbalimbali, hivyo inakufanya kuwa na machaguo mengi kila siku kulingana na hitaji lako.

**Viatu Sahihi**

Kila mfanyakazi anapaswa kuhakikisha ananunua viatu vinavyofaa ambavyo unaweza kuvaa ukiwa ofisini.

Ikiwa unavaa nguo za biashara katika ofisi, unapaswa kuhakikisha unavaa viatu vizuri.

Unashauriwa kwa kazi za ofisini ni muhimu kuvaa aina ya kutumbukiza vya ngozi, vinavyong'arishwa kila mara.

**Mapambo ya ziada**

Katika kuweka mazingira ya utanashati zaidi, unaweza kuongeza mapambo kama vile saa ya mkononi, kufunga tai na kuvaa miwani.







URB EMBO

Na Mary Geofrey

# NYWELE NYEUSI

SIKU hizi ni kawaida kuona watu wamepaka piko kichwani ili kuzifanya nywele zao ziwe nyeusi.

Leo tunaelekezana njia rahisi na sahihi ya kuzifanya nywele zako ziwe nyeusi bila kuongeza rangi ya ziada.

Njia hii ni nzuri na salama ya kufanya nywele kung'ara na kujaa kichwani.

Kabla ya kuanza kueleza namna ya nywele kuwa nyeusi, tujikumbushe sababu zipi zinafanya nywele ziwe nyekundu au nyepesi.

Sababu kubwa ni matumizi ya mafuta yenye kemikali na dawa za nywele ambazo hupoteza rangi halisi huwa nyekundu.

Kadhalika kutumia moto mara kwa mara kama vile kublowdry, kupasi na kunyoosha nywele kwa kutumia moto.

Katika mazingira hayo unaweza kutumia vifuatavyo ili kurudisha rangi halisi ya nywele.

**Baking soda**

Hii inatumika baada ya kusafisha nywele zako na kuwa safi.

Pima vijiko vitatu vya chai (vile vidogo) vya baking soda na unachanganya na maji.

Unachanganya vizuri mchanganyiko wako na unatumia kuoshea au kusuuzia nywele.

Hii inasaidia sana katika kuleta rangi halisi ya nywele.

**Asali na mafuta ya mzeituni**

Hii inasaidia kwa wale ambao wana tatizo la muwasho au kupata tatizo kichwani na nywele zikakatika bila kujua.

Chukua asali vijiko viwili na pima na mafuta ya mzeituni nusu kikombe.

Changanya vizuri, paka kwenye eneo lenye tatizo na unaweza kuvaa kofia maalum au ukaacha wazi.

Acha kwa muda wa dakika 20 hadi 30, kisha safisha kwa maji ya baridi.

**Papai:**

Hili linasaidia kwa watu wengi maana wakishaweka dawa kichwani huwa wana tabia ya kutaka kuzikata ili wazilinganishe na salon, lakini kwa kutumia papai ina uwezo wa kuzifanya nywele zako zilingane.

Chukua mtindi kiasi, papai nusu, vichanganye kwa pamoja, kisha paka mchanganyiko huo kwenye nywele zako, vaa kofia maalum na ukae kwa muda wa nusu saa, kisha osha kwa maji ya vuguvugu.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Tengeneza Ice Cream nyumbani

ICE cream ni aina ya chakula kama kiburudisho na inaweza kuliwa na watu wa rika zote.

Pia unaweza kula muda wowote utakaojisikia na ukafurahia maisha

**Jinsi ya kuandaa**

Maziwa fresh ml 240, sukari ml 240, chumvi kijiko kidogo cha chai robo, vanilla ya maji kijiko kikubwa cha chakula na vanilla ya mti ml 120.

Maziwa ya mafuta ml 120, Whipping cream yenye ubaridi wa wastani ml 480, biskuti zilizochovywa na chocolate ml 480.

Badala ya biskuti zilizochovywa na chocolate cream unaweza weka vipande vya chocolate, unaweza weka mchanganyiko wa ladha mabalimbali mfano matunda kama strawbery, chery, embe kwa kuchanganya kiasi cha ml 480.

Vunja vunja vipande vya biskuti vilivyochovywa na chocolate weka pembeni.

Weka maziwa katika sufuria nzito kwenye jiko lenye moto wa wastani acha yachemke mpaka yatakapotoa mapovu pembeni ya sufuria yaipue, weka sukari, chumvi na koroga viyeyuke.

Changanya tena whiping cream na vanila kwenye maziwa, kisha changanya maziwa na ile cream vilivyobaki hadi vichangayike vizuri.

Kisha mimina mchanganyiko wako wote kwenye bakuli safi la kioo ili uweze kupoa na kuganda chukua bakuli jingine kubwa kiasi ya lile lenye mchanganyiko wako kwa ajili ya kugandisha kuwa ice cream.

Weka barafu katika bakuli hilo kisha weka juu yake bakuli lenye mchanganyiko wako.

Baada ya mchanganyiko wako kupoa kabisa chukua mfuniko na funika bakuli vizuri na weka katika friji kwa saa nne au hata saa 24.

Baada ya hapo toa mchanganyiko wako kwenye friji kisha koroga vizuri na mwiko safi au kijiko kikubwa.

Funika tena na mfuniko ili kuzia hewa kuingia katika bakuli lako tayari kwa kugandisha kwenye jokofu.

Baada ya ice cream yako kuwa imeganda vizuri chukua zile biskuti zenye chocolate tupia katika mchanganyiko na uchanganye vizuri.

Kisha chukua chombo cha plastiki kisafi na kikavu, weka mchanganyiko



wako ndani yake na hakikisha unaacha nafasi ya inchi moja kwa ajili ya kutanuka.

Kisha funika vizuri na mfuniko safi na urudishe katika jokofu kuganda kabisa mpaka itakapokua ngumu.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Hizi ndizo sababu za kutokea nyufa kwenye nyumba

NYUFA kwenye nyumba ni miongoni mwa matatizo ambayo huweka doa ustawi wake.

Tatizo la nyufa ni moja ya magonjwa sugu yanayosumbua majengo na miundombinu mingine kwenye ujenzi, haijalishi ni jipya au la zamani.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Razack Jabir, anasema nyufa wakati mwingine hutokea kwa namna ambayo ni vigumu kuzuilika kutokana na mazingira au muundo wa ubunifu na usanifu wa muhimili wa jengo lenyewe.

Jabir anasema miongoni mwa sababu kuu zinazochangia kuwapo na nyufa kwenye nyumba au jengo ni kutitia na kwamba ni jambo la kawaida hasa kwa yale ambayo hayana muda mrefu baada ya kujengwa.

Anasema hali hiyo husababishwa na udhaifu wa msingi kushindwa kuhimili uzito wa jengo, kusinyaa na kutanuka kwa udongo uliobeba msingi wake, kuoza kwa baadhi ya mimea au viumbe vilivyopo chini ya ardhi, kukua au kuoza kwa mizizi ya miti na mabadiliko ya hali ya hewa kwa kutegemea asili ya mazingira ya eneo husika.

Anasema nyufa hutokea zaidi pale upande mmoja wa jengo unapotitia na upande mwingine kubaki katika hali yake tatizo ambalo hutokea kwa kutegemeana na ubora na umakini wa matokeo halisi ya upembuzi yakinifu wa kisanifu kabla ya ujenzi.

Jabir anasema ni muhimu sana kufanya uchunguzi wa kisanifu kwenye eneo husika kabla hujaanza ubunifu na usanifu wa kile unachokwenda kujenga ili kuepukana na nyufa baada ya ujenzi.



Sababu nyingine ya nyufa anasema ni kutokidhi vigezo vya usanifu na ubunifu majengo.

Kwamba mabadiliko ya haraka ya teknolojia ya uhandisi yanayoendelea kutokea duniani yanawaacha nyuma baadhi ya wataalamu wa ujenzi, hali ya uchumi na ubora wa vitendea kazi ni vikwazo kwa baadhi ya wataalamu wa ujenzi.

Anasema ubunifu na usanifu majengo ni jambo mtambuka linalohitaji uwezo na ujuzi wa hali ya juu sana tofauti na wengi wanavyofikiri na kwamba kazi hiyo ni muongozo wa utendaji katika kila hatua wakati wa ujenzi.

Anasema kutokidhi vigezo vya ubunifu na usanifu majengo ni rahisi sana kutengeneza matatizo kwenye majengo yanayokuwa yanajengwa.

## Namna ya kupamba meza kwa matunda



Katika kupendezesha meza yako ya chakula, unaweza kutumia matunda kama pambo la kuwavutia walaji.

Kama umepata wageni muhimu tafuta njia ya kuwapa hamu ya kula chakula chako. Hizi ni baadhi ya dondoo muhimu za namna ya kupendezesha meza ya chakula kwa matunda.


1: Panga sahani ndogo na matunda kwenye meza, matunda yanayofanana changanya na mengine, usiondoe maganda.

2: Tenganisha zabibu kwenye mafungu madogo, matufaa kata katika vipande vya nusu mwezi. Pia machungwa yamenywe na kukatwa.

3: Chagua matunda magumu, sio laini na ambayo hayakuiva zaidi, ni rahisi kula bila kukata. Hakikisha matunda yote yamekatwa isipokuwa ndizi. Tikiti maji, linaweza kukatwa vipande vidogo.

4: Panga matunda yaliyomenywa katika sahani ndogo kuzunguka kila saani ya chakula ya kila mmoja, hakikisha matunda yasiyomenywa yapo katikati ya meza ili kuweka mvuto zaidi.

# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
'MWOKOZI NTUPIE JICHO!'
SISI
UKAME
LAKINI MSHENGA HAUWAWI ILA WEWE UNATAKA KULETA NONGWA KISA BINTIYO DARASA LA SABA!
MSHENGA WEWE UTAUWAWA MAPEMA SANA KWA SHOBO ZAKO! UTAFANYA USHENGA HADI KWA MKEO!
NDIO MMEPATIA SABABU YA KUACHA KUKOGA NA KUFUA, HADI MNAKUJA HUMU KUBANANA TUNANUKISHANA MIJASHO TU!
WE MPUUZI KWELIKWELI UNATAKA UWE MREMBO WAKATI MAJI YA SHIDA!
HUYO ANAPENDA SIFA BILA KUJALI KUWA KUNA UKAME
UKAME UWE MCHAFU?
NALO NENO!
HAKUNA ANAYEPENDA KUWA MCHAFU WEWE!!! ANGALIA MIE HATA NGUO SIJANYOOSHA KISA UMEME
NADHANI TURUDI KWENYE MILA ZETU TUANZE MATAMBIKO MVUA ZINYESHE
LABDA MKATAMBIKE BAR, MAANA MITI MIKUBWA YOTE IMEISHA KWA KUPASUA MBAO!
MPENZI NATAKA LAKI SITA KODI IMEISHA, ALAFU LEO NATAKA REJESHO UNIPE PIA
HALI HII NI MKE WA MTU, ANGEKUWA SINGO SIJUI NINGEPUMULIA WAPI?
MKE WANGU NASKIA KABATI LETU...ETI UMEMTUNZA MAMA SIWATU KWENYE KICHENIPATI...?
MWANAUME HUWA HAPENDEZI KUITWA 'MPASHUKUNA AU MSHAKUNAKU' KWANI KABATI ULILINUNUA WEWE AU SHOBO?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
SIFA YA BATA NDIO UTAMU WA NYAMA YAKE...

## HABARI KIMATAIFA

# Kenyatta, Kagame kuwashinikiza M23

**NAIROBI,** KENYA

RAIS wa zamani wa Kenya Uhuru Kenyatta na Rais wa Rwanda, Paul Kagame wamekubaliana kuhusu haja ya waasi wa M23 kusitisha mapigano na kujiondoa katika maeneo ya mashariki mwa Congo.

Jumuiya ya Afrika Mashariki ilithibitisha kuwa viongozi hao wamekubaliana namna ya kuwashinikiza waasi hao kuondoka haraka katika maeneo wanayoyakalia.

Mwaka huu, waasi wa M23 wameendesha mashambulizi kadhaa mashariki mwa Congo, ikiwa ni kurejea kwao kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2012, na kusababisha makabiliano na jeshi la Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na maelfu ya raia wamelazimika kuyahama makazi yao tangu mwezi Machi. Machafuko hayo yalizua mvutano wa kidiplomasia kati ya DRC na Rwanda, kwa kila upande kuutuhumu mwenzie kuwaunga mkono makundi ya waasi.

Kenyatta aliitembelea Congo wiki hii akiwa kama kiongozi wa usuluhishi wa wajumbe saba wa Jumuiya ya EAC na mjumbe wa amani wa Umoja wa Afrika.

Alifanya mikutano mjini Kinshasa na aliwatembelea wakimbizi wa ndani waliouhama mji muhimu wa mashariki wa Goma, ambako M23 wamekuwa wakiukaribia. Aliporejea, Kenyatta alizungumza na Kagame kwa njia ya simu na kukubaliana kusitisha mapigano mara moja.

Kulingana na taarifa za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kagame alikubali pia kumsaidia Kenyatta kuwahimiza waasi wa M23 kuweka silaha chini na kujiondoa katika maeneo waliyoyanyakua na kuyadhibiti.

Mbinu za kufanikisha hatua hiyo zitajadiliwa wakati wa duru ya pili ya mazungumzo katika mji mkuu wa Angola Luanda wiki ijayo.


Naibu msemaji wa Rais wa Congo Felix Tshisekedi ameliambia shirika la habari la Reuters, kuwa hatua hiyo inatia moyo kuona Paul Kagame ametambua kuwa anaweza kuwashawishi M23, na kuongeza wanasubiri kuona kitakachotokea katika uwanja wa vita.

Msemaji wa serikali ya Rwanda hakuzungumzia mara moja taarifa hiyo.

Ilipoundwa mnamo mwaka 2012, M23 lilikuwa kundi jipya zaidi lililoibuka katika safu ya makundi mengine yanayoongozwa na Watutsi ambayo yalianzisha uasi dhidi ya vikosi vya Congo.

Waasi waliteka maeneo mengi mwaka 2012 na kwa muda mfupi waliushambulia mji wa Goma kabla ya kutimuliwa na wanajeshi wa Congo wakisaidiwa na vikosi vya Umoja wa Mataifa na kukimbilia katika mataifa jirani ya Uganda na Rwanda mwaka uliofuata. M23 wamefanya mashambulizi matatu makubwa tangu mwezi Machi. Marekani, Ufaransa, Uingereza na Ubelgiji zimelaani kwa maneno makali kusonga mbele kwa waasi wa M23 mashariki mwa DRC, na kuwataka warudi nyuma mara moja na kusitisha uhasama.

**DW**



Kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un akiwa na binti yake Kim Chu-ae wakati wa uzinduzi wa makombora ya masafa marefu juzi: **PICHA KCNA/REUTERS**

# Kim Jong un amwonyesha hadharani binti yake

**PYONGYUNG,** KOREA KASKAZINI

KIONGOZI wa Korea Kaskazini Kim Jong-un, kwa mara ya kwanza ameonekana hadharani akiwa na binti yake mdogo na kuthibitisha ripoti za muda mrefu za kuwepo kwa mtoto huyo.

Msichana huyo, anayeaminika kuwa ni Kim Chu-ae, aliungana naye katika ukaguzi wa kurusha kombora kubwa la masafa marefu siku ya Ijumaa.

Wawili hao walisimama wakiwa wameshikana mikono wakati jaribio hilo likitekelezwa.

Jaribio hilo lililaaniwa vikali na mataifa ya magharibi.

Kim anaongoza mojawapo ya mataifa yenye siri zaidi duniani, na masuala machache yanajulikana kuhusu maisha yake ya binafsi.

Picha kadhaa zilichapishwa na shirika la habari la serikali ya Korea Kaskazini KCNA, ziliwaonyesha wawili hao wakiwa wameshikana mikono huku wakizungumza na maofisa wakati wakikagua makombora na kutazama uzinduzi huo.

Michael Madden, mtaalam wa Korea Kaskazini kutoka Kituo cha Stimson huko Washington, alisema anaamini Chu-ae alikuwa na umri wa kati ya miaka 12 na 13. Alisema kuonekana hadharani kunaweza kuwa njia ya Kim ya kuonyesha kwamba kizazi cha nne cha mrithi wa mamlaka kitakuja kupitia kwake.

Mnamo Septemba, wataalamu kadhaa wa Korea Kaskazini waliripoti kwamba Chu-ae alionyeshwa kwenye video kwenye sherehe za siku ya kitaifa nchini humo.

Hata hivyo, ilikuwa ni uvumi, na uongozi wa Korea Kaskazini haukuthibitisha kuwa ni binti wa kiongozi huyo.

**BBC**

# Nusu ya mifumo ya umeme imeshambuliwa Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

SERIKALI ya Ukraine imesema mashambulizi ya makombora ya Russia yanayoendelea kutupwa kila kukicha, yameathiri karibu nusu ya mifumo yake ya nishati ya umeme.

Hata hivyo, viongozi wa mji mkuu wa Kyiv walionya kwamba jiji hilo linaweza kukabiliwa na kukatika kabisa kwa gridi ya umeme wakati huu wa msimu wa baridi. Katika miezi tisa ya vita, Russia imeendesha mashambulizi makubwa zaidi nchini humo na kuilenga miundombinu ya kiraia.

Katika hotuba yake jana usiku, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy alisema kuwa karibu watu milioni 10 hawana umeme nchini humo.

Umoja wa Mataifa ulisema uhaba wa umeme na maji nchini Ukraine unatishia kutokea kwa maafa makubwa ya kibinadamu katika msimu huu wa baridi.

**DW**

# Mwendesha mashtaka maalum kumchunguza Donald Trump

**WASHINGTON,** MAREKANI

MWANASHERIA Mkuu wa Marekani Merrick Garland, amemteua mwendesha mashtaka, Jack Smith, ili kufanya uchunguzi ulio huru dhidi ya rais wa zamani Donald Trump, siku chache baada ya kutangaza nia yake ya kugombea tena Urais katika uchaguzi wa mwaka 2024. Garland alisema uchunguzi huo ni kwa manufaa ya umma ili kuendeleza kesi mbili zinazomkabili Trump ambazo ni juhudi za kiongozi huyo wa zamani kutaka kubadili matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2020 na usimamizi wake kwa nyaraka muhimu za Ikulu.

Trump amelaani hatua hiyo na kusema ni uamuzi wa kisiasa na usio wa haki kwa sababu tu anaongoza katika kura ya maoni, huku akibainisha kuwa kamwe hatotoa ushirikiano kwa timu ya uchunguzi.

Utawala wa Rais Joe Biden ulisema hautaingiza siasa katika maswala ya sheria,

**DW**

## MAKALA

# TUELIMIKE BADALA YA KUSTAARABIKA



Na Magabilo Masambu

KUPATA elimu ni jambo la msingi na la muhimu sana katika maisha ya kila mwanadamu, hasa katika maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Elimu inapaswa kutafsiriwa kwa vitendo katika shughuli za maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Tukishindwa kuitumia elimu katika kubadili mawazo na fikra, kwenda kwenye vitu vinavyoshikika basi hatutakuwa na faida na elimu yetu.

Katika taifa letu, vijana au makundi ya watu wamepata elimu ya kutosha lakini yawezekana kuelimika bado limekuwa tatizo kubwa. Hii ni kwa sababu, kupata elimu na kuelimika ni mambo mawili tofauti ambayo jamii inabidi ianze kutambua. Tatizo hili limejitokeza kwa sababu ya kutotambua kusudi halisi la elimu na matumizi yake katika maisha yetu.

Dhana ya kusoma sasa ni kujaribu kufanya jitihada ili kuyakwepa matatizo na kuongeza kipato lakini tumejikuta hatutengenezi ujuzi. Badala yake tunatengeneza wasomi waliostaarabika bila kuelimika. Ustaarabu tunaouzungumzia hapa pia ni ule wa kuzikataa mila zetu baada ya kupata elimu. Inawezekana ni mzuri sina tatizo nao, lakini elimu yetu ingetufanya tuelimike zaidi kwa kuitumia katika kujenga uchumi wetu na wa taifa.

Kupata elimu na kuelimika vyote vimetawaliwa na nguvu ya fikra na uamuzi. Ili mtu aelimike, anapaswa afanye uamuzi wa kuitumia elimu yake katika maisha halisi kwa kuyatumia mazingira yake yanayomzunguka ili kuimarisha maisha yake na ya wengine pia. Vijana wengi baada ya kuwa wamepata elimu, wamekuwa wakijua tayari wameshaelimika kwa sababu wanavyo vyeti tayari, kumbe elimu ili ilete faida ni lazima watu waitumie katika maisha yao ya kila siku.

Ukiweka mafuta kwenye gari na ukaacha kuyatumia gari halitaondoka. Ukiwa na elimu, lakini ukawa hujaelimika maana yake matumizi yake hayataonekana. Badala yake unaweza kuitumia kujidai tu na kutishia watu vyeti vyako ulivyobandika ukutani ili kila anayeingia ndani kwako ajue unazo shahada kadhaa. Tunataka hizo shahada zionekane kwenye fikra na matendo yako.

Kusudi kuu la elimu ni kupata maarifa yanayoifanya akili inyambulike kwa urahisi zaidi, juu ya kutenda shughuli mbalimbali ambazo mhusika anahitaji kufanya katika maisha yake. Mfano, mtoto wa kike anapopata elimu kuhusu mapishi, tunataka tuone chakula kizuri. Kama ni ugali ni mjuzi wa kuupika kwelikweli na kama ni samaki amepikwa kwa ustadi na kuiva vizuri. Hapo tutasema amepata elimu na kuelimika.

Ni ukweli kwamba katika nchi yetu kuna baadhi ya vijana wasomi si wote ni wachache, walioamua kuelimika na kwa sasa wameamua kuiwekeza elimu yao katika mambo ya kiuchumi, kuendesha maisha yao na kuzalisha ajira kwa Watanzania wengine. Mfano kilimo cha kisasa na viwanda vidogo vidogo vya usindikaji kupitia mikopo na ruzuku mbalimbali kutoka serikalini, hao tunawapongeza kwa dhati kabisa.

Wakati vijana hao wachache walioamua kuitumia elimu kuendesha miradi yao mbalimbali, baadhi ya vijana wengine wanaojiita wasomi, wenye elimu bila matumizi, wamejikita wakidharau shughuli za kujiajiri kutoka kilimo na baadhi ya kazi nyinginezo za kimaendeleo.

Leo hii wako baadhi ya wasomi ambao wamekataa hata kuongea lugha za makabila yao kwamba ni kujiaibisha kwa sababu wamestaarabika, anasalimiwa na ndugu yake kikabila anaitikia kwa kiswahili ili asionekane mlughalugha katoka kwao sitimbi!

Wengine hata wanapokuwa wanasubiri matokeo yao ili kuendelea na masomo, huona vigumu hata kwenda mashambani kusaidia wazazi wao wakati shamba ndilo limefanya akapata ada na matumizi mengine. Hilo ni jibu tosha kwamba vijana wengi wako katika ulimbukeni kuwa elimu ni kuja kuajiriwa ofisini, jambo ambalo si kusudi kuu la elimu. Tukitafakari mchawi ni nani katika hili suala nyeti nchini, majibu kamili ni jamii yetu kiujumla kukosa ufahamu dhabiti kuhusu matumizi sahihi ya elimu.

Serikali ianzishe mpango mkakati imara katika kuwasaidia vijana kwa kuwatengenezea mazingira mazuri katika kuanzisha, kuendeleza na kukuza vipaji na miradi yao mara baada ya vijana hawa kuhitimu elimu zao.

Mazingira hayo ni pamoja na kuweka kipaumbele katika wizara ambazo zinaweza kutengeneza vijana wengi kujiajiri na kuwarahisishia mifumo ya masoko na mitaji, kupitia ruzuku na mikopo ya serikali ama mabenki binafsi nchini.

Vijana ni nguvu kazi chanya kwa taifa letu endapo tu wakiandaliwa mazingira bora. Kinyume na hapo, vijana hawa wanaweza kuwa nguvu kazi hasi kwa taifa, ikiwa serikali haijawaandalia mazingira bora, nguvu ambayo inaweza kurudisha taifa nyuma kwa kasi kubwa na kuangamiza kizazi na kizazi.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Mambo Iko Huku', 'Mtu Mzima Ovyo' zilivyowapaisha Khadija Kopa, Nasma



Na Adam Fungamwango

**Khadija Kopa, Malkia wa Mipasho na Nasma Khamis 'Kidogo' waliyapamba makundi haya kwa nyimbo mbalimbali ambazo ziliufanya muziki wa taarabu kuwa tishio kwa aina zote za muziki zilizokuwapo nchini wakati huo.**

ILIKUWA patashika nguo kuchanika kwenye kumbi mbalimbali za burudani miaka ya 2000 hadi katikati pale makundi mawili hasimu wakati huo, Tanzania One Theatre (TOT) na Muungano Cultural Troupe yalipokuwa yakiamua kushindana.

Makundi hayo ambayo yalikuwa na idara tofauti ndani ya kundi moja kama vile ngoma za asili, vichekesho, maigizo, sarakasi, taarabu na hata muziki wa dansi, yalikuwa yakiweka mipambano ambayo ilikuwa ikivutia mashabiki wengi wakati huo, wakiwa wamegawanyika pande mbili mithili ya mashabiki wa Simba na Yanga. kilichowagawanyisha zaidi ni muziki wa taarabu ambao wakati huo ulikuwa kwenye kilele cha mafanikio.

Kumbi zilifurika mashabiki kibao kwenda kushuhudia pambano kati ya TOT iliyokuwa ikiongozwa na Kapteni John Komba upande mmoja na Nolbert Chenga upande wa Muungano. Kundi hili lilikuwa na kitu cha ziada ambacho baadhi ya makundi yalikuwa hayana, nacho ni maonyesho ya nyoka, hasa aina ya chatu.

Tukirudi kwenye taarabu, ndiyo iliyafanya makundi haya kuwa maarufu zaidi, Khadija Kopa akiwa upande wa TOT na Nasma aliyekuwa upande wa Muungano. Kwa hali ya kawaida hata mashindano yao kwenye kumbi mshindi alikuwa hapatikani. Ni kwamba mashabiki wanakuwa wamegawanyika nusu kwa nusu.

Kikubwa kilichokuwa kinafanyika pale ni biashara kwani walikuwa wanakusanya mashabiki wengi mno. Ilikuwa biashara kubwa ya muziki wa taarabu ambayo haijawahi kufanyika nchini. Huku mtaani pia kulikuwa na mabishano kuwa nani zaidi kati ya TOT na Muungano. Ni kama Simba na Yanga tu, mshindi huwa hapatikani kwa kubishana.

Kwenye redio, hasa Radio One na kipindi chake cha 'Nani Zaidi' walikuwa wakiwapambanisha na kusababisha mchuano mkali wa simu zinazomiminika. Mara kwa mara mshindi alikuwa hazidi kura tano kila upande.

Khadija Kopa, Malkia wa Mipasho na Nasma Khamis 'Kidogo' waliyapamba makundi haya kwa nyimbo mbalimbali ambazo ziliufanya muziki wa taarabu kuwa tishio kwa aina zote za muziki zilizokuwapo nchini wakati huo.

Kuna wakati taarabu ikachomoza kuwa aina ya muziki pendwa zaidi nchini na kutengezwa vipindi mbalimbali vya muziki huo tu kabla ya nyimbo zao za kuzodoana na vijembe ambavyo vilikuwa ni kwa uhasama zaidi ya ushindani wa kibiashara, waimbaji hao tayari walishakuwa maarufu kutokana na nyimbo mbalimbali ambazo walizitoa.

Kasheshe ilikuja pia pale Kopa alipoondoka kwenda nchini Oman baada ya kupata mkataba. Inasemekena walianzisha kundi lao la taarabu, lakini aliporudi nchini uongozi wa TOT ukakataa kumpokea. Akajiunga na Muungano ambako alimkuta hasimu wake Nasma.

TOT nao kuona hivyo, wakaona isiwe taabu, wakatumia nguvu kubwa kumchomoa Nasma kutoka Muungano naye akajiunga na TOT. Hii iliwachanganya mno mashabiki wa taarabu. Kwa sababu kulikuwa na mashabiki wa bendi, halafu kukawa na mashabiki wa Khadija na Nasma. Ikawagawanya tena. Ikarudisha upya upinzani wa waimbaji wao na makundi yao na maonyesho ya pamoja kwa ajili ya kupambana yakazidi kuchukua chati. Baadaye sana, Khadija alirejea TOT.

Twende sasa kwenye nyimbo ambazo ziliwafanya kuwa juu kama mgomba wa ndizi na kuchukuliwa kuwa ndiyo moja kati ya waimbaji taarabu wachache nchi hii waliokuwa maarufu zaidi.

Khadija aliibuka na kibao matata 'Mambo Iko Huku' ambacho kilizua misamiati, misemo ya mizaha mitaani na kila kitu.

"Umekwisha umepwaya hoi waranda na njia, umebaki sura mbaya, mkogoro utakuua. Akutake nani wewe, akusifu nani wewe, ondoka kisirani wewe

Je taarabu ipo hapo, taarabu imo humo? Aipate wapi? Huyo kibuzi marika mtazame anavyojitikisa, sijali lolote, wewe, mambo iko huku.

Na kwenye mambo humo. Katika wenye taarabu humo, umebaki mchomo hata nywele huna, wingi wa kikomo. Waenda saluni si saizi yako, waachie wenye fani bibi, hasara kwako, nywele za kilioni ndiyo saizi yako."

Ni baadhi ya mashairi yaliyomo kwenye wimbo huo wa TOT.

Nasma naye, akiwa na Muungano akatoka na kibao alichokiita 'Mtu Mzima Hovyo'.

Achia ngazi bibi mchuma unaondoka huo. Umepwelea naondoka naye, umeishiwa ninadunda naye, kipi cha kung'ang'ania, hakutaki hebu timua. Mtu ovyo unajishaua, unajisumbua.

"Si zaizi yako wewe, unajilengesha hakutaki, kaona mambo yako huku taarabu imo kaona mambo yako huku, we, utaumiza roho yako. Naringa hutomchukua mambo yangu yameshamzingua, kaona mambo yako huku taarabu imo we, utaumiza roho yako." Huyo ndiye Nasma.

Khadija naye akaja tena na 'Mtie Kamba Mumeo. "Kama unaweza mtie kamba mumeo umzuie, ukitahamaki chini kachimba mumeo ninae mie. Ninae mie natamba naye.

Mbio kanikimbilia, akaniomba mapenzi, nami nikamringia, kanizingua kichizi, nami nikamridhia, kila kitu la azizi. Nikamwambia chukua upendacho la azizi."

Nasma ambaye alifariki dunia mwaka 2009, akaja na wimbo wenye mashairi haya.

"Bure utajikondesha na kujipa taharuki, eti wajifaharisha, yeye unammiliki, mimi nakufahamisha, mahabuba hakutaki, kichekesho wachekesha masikini hujijui, kwake wajitamanisha, hakutaki koroboi."

Mambo yaliendelea hivyo, hadi walipomalizia na nyimbo kadhaa zikiwemo 'Niliwaze' 'Sanamu na Michelini' na kadhalika.

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi imevunjika-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

GHAFLA akakunja sura alipoona namba ya mtu huyo ambaye simu yake inalia. Akaiweka mezani. Hakutaka kupokea kabisa. Akikumbuka kisa cha kuitwa Kibaha na kwenda kuambiwa mambo ambayo aliona yasingewezekana, hakutaka tena kusikia habari za huko. Ni sehemu ambayo ilikuwa chungu kwake. Hakutaka hata kuisikia.

Ikakata, lakini baada ya dakika mbili ikapigwa tena. Akili nyingine ikamjia kuwa apokee, lakini akatae atakachoambiwa. Ilikuwa ni namba ya mzee Mbegu. Akabonyeza kitufe cha kupokelea. Haraha haraka akaanza yeye kusalimia

"Shikamoo babu."

"Marahaba mjukuu wangu, habari za siku mbili tatu?"

"Nzuri mzee, wanasemaje huko?"

"Aaah bwana huku habari siyo nzuri."

"Eee, unasema?"

"Habari huku siyo nzuri shemeji yako Zulfa ameumwa na nyoka."

"Duh, kweli babu siyo habari nzuri hizo, enhee ilikuwaje na mmempeleka hospitali?"

"Mjukuu wangu, tumetumia dawa za kienyeji hapa, tumemchanja, tumefanikiwa kutoa sumu, sawa kwa hilo imefanikiwa, lakini sasa naona mguu kama umeanza kubadilika rangi unakuwa mweusi."

"Hee, sasa babu mmemuwahisha hospitali?" "Wakwe zako na ndugu wamempeleka kwa mganga wa kienyeji, wanasema amerogwa."

"Mama yangu! Watamkosa huyo mtoto au binti anaweza kuukosa mguu wake mkileta mchezo, huyo apelekwe hospitali." "Nina nguvu hiyo mjukuu wangu? Labda uje wewe unisaidie."

"Haya babu nitaangalia."

"Usiangalie mjukuu wangu, huku mimi naona wewe na mimi ndiyo akili zetu zinafanana hawa wengine huku akili zao wanazijua wenyewe."

"Haya babu nitakuja."

"Nitashukuru sana."

Simu ikakatwa. Jerry akaingia tena kwenye mtihani mwingine. Mtihani wa kwenda tena sehemu asiyoipenda, Kibaha. Mara nyingi akienda huwa hawaambii ndugu zake, hasa dada zake kwani anatambua kuwa anaweza kupewa maneno ya kuudhi.

Kwenda sehemu ambayo imewadhalilisha. Imewafedhehesha na kuwatia aibu ukoo mzima, leo ionekane kuwa yeye anakwenda kila baada ya wiki moja.

Habari za Zulfa kupata matatizo ya kuumwa na nyoka zilimfanya kufikiria kwenda kutoa msaada. Msaada ambao




**"Habari ndiyo hiyo kijana, yaani hapa ninavyokwambia kuna ugomvi mkubwa baina ya familia mbili, ya mama Zulfa na mama Said. Kinachoonekana hapa ni kama vile mama Said alimuapiza Zulfa kuwa ataona baada ya kumkataa kijana wake Said.**

utamuwezesha kupata matibabu sahihi na siyo kama aliyoyasikia kwa mzee Mbegu.

**************************************

"Habari ndiyo hiyo kijana, yaani hapa ninavyokwambia kuna ugomvi mkubwa baina ya familia mbili, ya mama Zulfa na mama Said. Kinachoonekana hapa ni kama vile mama Said alimuapiza Zulfa kuwa ataona baada ya kumkataa kijana wake Said. Mama yako naye baada ya kuambiwa hivyo akaenda huko huko, ukazuka ugomvi si wa kawaida, mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Matibabu pekee aliyopata ni kumchanja na kuweka dawa ya kunyonya sumu." Mzee Mbegu alitiririka.

"Poleni sana babu, sasa tunafanyaje?"

"Nadhani wewe ndiye utakuwa mwanaume pekee unayeweza kusawazisha hili. Yote yametokea kwenye familia hii, kuanzia habari za Vayajo mpaka za Zulfa. Vayajo alikukimbia, Zulfa naye akakataa kuchukua nafasi ya dada yake. Sasa hii ndiyo fursa kwako ya kuionyesha familia hii kuwa wewe ni mtu muhimu. Wewe si kijana wa kawaida kama walivyokuwa wanakuona. Kuwa mtu wa pekee ambao wao hawajawahi kumuona, inaweza ikakulipa."

Maneno ya mzee Mbegu, ambaye ni babu wa Vayajo na Zulfa yalimuingia Jerry na kwa mbali ni kama alianza kumuelewa. "Sawa babu, nimekuelewa, nitafanya kama inavyotakiwa kufanya, ila naomba unisaidie pale ninapohitaji msaada."

"Haina tatizo, sasa tutoke hapa nyumbani kwangu, twende tukamuone mgonjwa."

Hakukuwa mbali sana. Ni kama nyumba tano tu kutoka pale. Waliingia ndani. Mama Zulfa alishtuka kumuona Jerry.

Lakini akaupoza mshtuko wake kwa kuwakaribisha, "karibuni wageni." Akawakaribisha huku akinyanyuka kwenye mkeka.

Ilibidi afanye hivyo kwa sababu waliokuwa wanaingia wa kwanza ni mzazi wa mumewe, mkwe, lakini pia upande wa pili kulikuwa na 'mkwe' mwingine ambaye ilikuwa amuoe binti yake Vayajo.

"Karibuni, mgonjwa yupo ndani." Waliongozwa kwenye chumba ambacho Zulfa alikuwa amelala. Jerry alimtazama akagundua ule urembo aliomuona nao wiki kadhaa zilizopita ulikuwa unaanza kupotea sababu ya ugonjwa. Akagundua kuwa inawezekana kutokula vizuri, maumivu na hofu vimechangia sana kusawajika.

"Pole sana Shem."

"Ahsante." Akajibu kwa sauti hafifu.

"Unajisikiaje sasa?" Akauliza tena.

"Sijambo kidogo, siyo kama zile siku za mwanzo." Jerry hakuwa na kizuizi, mgonjwa ni shemeji yake, alichofanya ni kufunua khanga aliyokuwa amejifunika, upande miguu ili aangalie ukubwa wa ugonjwa wenyewe.

Hali haikuwa nzuri sana. Mguu ulitengeneza kama rangi ambayo ilikuwa tofauti na mguu wa pili. Kuna sehemu yenye kiduara kidogo ambayo ilikuwa nyeusi. "Hapa ndipo alipokuuma?"

"Ndiyo, hapo hapo."

"Zulfa, hapa inaonekana hujapata matibabu halisi ya ugonjwa huu. Mimi naomba nikuchukue nikupeleke hospitali." Jerry akaamua kulisema hilo bayana.

"Mimi sina neno, ninachotaka ni kupona tu, nimeshatolewa sumu mguuni, nimeshapelekwa kwa mganga wa kienyeji, hata wewe ukinipeleka hospitali sina la kusema. Ila tu mwambie mama."

Mzee Mbegu alimkaribia Jerry na kumnong'oneza kitu ambacho hata Zulfa hakusikia.

"We ongea na mama yake tu, akikubali tu basi fursa ya kumpeleka hospitali imekamilika, baba yake huyu hana la kusema mbele ya mkewe. Mke hapa ndiyo kila kitu."

Baada ya kumaliza kumnong'oneza, akaita kwa sauti. "Mama Zulfaaa." Sauti ya kuitikia ikasikika upande wa pili nje "Beee" Sekunde kadhaa baadaye aliingia na kuketi chini ya sakafu.

"Mama mimi nimekwita hapa. Tusema tu nimemuangalia shemeji yangu hapa, hali yake si nzuri sana. Ni kweli mmejitahidi kwa kila hali ili kumfanya arudi kwenye hali yake ya kawaida. Lakini kuna sehemu bado haijafikia. Anahitaji matibabu zaidi huyu ili mguu wake urudi kama zamani. Kwa hiyo apelekwe hospitali huyu." Mama aliinamisha kichwa chake kama anafikiri kitu hivi. Akashusha pumzi.

"Ni kweli mwanangu, hata mimi mama yako na baba yako tulikuwa na wazo hilo, lakini pesa yenyewe ya matibabu ya kumudu hilo hatuna, pili hili baba siyo la hospitali, ni michezo tu ya watu, wamemroga, kuna kijana alikuwa anataka kumuoa, akakataa, ndiyo mama yake akamfanya hivi."

"Sawa mama, mimi sitaki kuingilia masuala yenu mnayoamini, lakini mimi naomba tu apelekwe hospitali, akirudi mtaendelea kupelekana kwa waganga na suala la gharama mimi nitagharamia matibabu yote, hata wakisema alazwe mwezi mzima."

Mama Vajayo alipatwa na mshtuko kidogo. Hakutarajia hilo. Mtu ambaye hivi karibuni amefanyiwa kadhia kubwa kama ile, leo anajibebesha mzigo wa gharama. Moyoni mwake hakutaka binti yake apelekwe hospitali kwa sababu aliamini amerogwa, lakini kutokana na heshima kwa kijana Jerry kuthamini mchango wake licha ya yote yale aliyofanyiwa na binti yake, akaamua kukubali.

"Sawa mwanangu, nimekubali."

Jerry aliwaangalia mzee Mbegu na Zulfa kwa zamu. Wote walitabasamu. Zulfa alionekana kupata imani ya kupona kwani alianza kukata tamaa ya kuishi.

**INAENDELEA JUMAPILI**

HABARI BURUDANI

# ASLAY ALAMBA DILI SONY MUSIC

HATIMAYE mwimbaji nyota wa Bongo Fleva, Aslay amesema ni bahati kwake kujiunga na lebo ya Sony Music Entertainment na kuwa miongoni mwa wasanii watakaonufaika na kazi zao.

Aslay ambaye jina lake halisi ni Isihaka Nassoro, ni msanii mwenye kipaji cha hali ya juu cha uimbaji na utunzi na kumfanya kuwa maarufu Afrika Mashariki.

"Nimebarikiwa sana kutangaza ushirikiano wangu na Sony Music Afrika. Hii ni fursa nzuri, si kwangu tu, bali kwa aina yangu ya muziki, Bongo Fleva! ambayo ninaipenda sana," amesema Aslay.

Awali Mkuu wa Sony Music Afrika Mashariki, Christine Mosha maarufu kama Seven, amesema kumpata msanii huyo ni jambo la kujivunia.

"Ninajivunia kuwa na msanii wa hadhi ya Aslay kuungana nasi katika Sony Music Africa, ni mwimbaji na mtunzi ambaye ametetea Bongo fleva kote barani Afrika." amesema





# NASLIM TZ KUJA NA MPANGO MPYA

Mwimbaji maarufu wa Kaswida nchini, Naslim TZ amesema kupitia kundi lake la Fanny Crew, amekuja na mpango kazi mpya aliloubatiza jina la Bunge.

Akizungumza na BT, Naslim alisema jukumu kubwa la mpango huo ni kuja na nyimbo zenye mwendelezo kulingana na matukio mbalimbali yanayotokea kwenye jamii ili serikali kuyafanyia kazi.

"Nimeshaimba kaswida muda mrefu sasa nimekuja na mpango wa bunge ambao nitafanya mimi na kundi langu la Fanny Crew, tutaangalia matukio kwenye jamii au kutoa ushauri na tutaigiza kama tupo bungeni ili serikali iweze kuchukua mawazo kupitia sisi," amesema Naslim.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

### TOURE ANUKIA WIGAN

KOLO Toure anatarajiwa kuteuliwa kuwa kocha wa klabu ya wa Wigan. Beki huyo wa zamani wa Manchester City, Liverpool, Arsenal na Ivory Coast mwenye umri wa miaka 41, kwa sasa yupo kwenye becnhi la ufundi la Leicester City. (***Sun***)

### GOSENS KUTUA LEICESTER

KLABU ya Leicester ina nia ya kumsajili beki wa kushoto wa Timu ya Taifa ya Ujerumani, Robin Gosens mwenye umri wa miaka 28 kutoka Inter. (***Calciomercato***)

### RONALDO KUSAJILIWA URENO

TIMU za Ligi Kuu Ureno zinatarajia kuwa katika nafasi ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 kutoka Manchester United. (***iNews***)

### BRUNO, RONALDO SAFI

BRUNO Fernandes amesema "hana tatizo" na mchezaji mwenzake wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo licha ya majibizano yasiyokuwa ya kawaida kati ya wawili hao kunaswa na kamera. (***Sky Sports***)

### PELLISTRI KUONDOKA UNITED

WAKALA wa mshambuliaji wa Manchester United na Uruguay, Facundo Pellistri, mwenye umri wa miaka 20 amesema mteja wake anaweza kuondoka Old Trafford Januari akiwa bado hajachezeshwa hata mechi moja katika kikosi cha kwanza cha timu hiyo. (***El Observador***)

### POCHETTINO AITAKA UNITED

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino amedokeza muda usiofaa ulimzuia kuwa Kocha wa Manchester United, lakini amesema uhamisho huo bado unaweza kutokea katika siku zijazo. (***Radio Marca***)

### BARCA KUMUUZA DEPAY

BARCELONA itamuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 28 ifikapo Januari. (***AS***)

### BELLERIN ATAJWA ROMA

JOSE Mourinho anataka kumleta beki wa kulia wa Barcelona, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 27 kwenda AS Roma. (***Gazzetta dello Sport***)

### WILSHERE HATAKI UTANI

KIUNGO wa zamani wa Arsenal na England, Jack Wilshere mwenye umri wa miaka 30 amesema atawapigia simu wachambuzi, kama vile Jamie Redknapp na Paul Scholes, ikiwa watamkosoa. (***Sun***)

### SAKA KUPIGA PENALTI

AARON Ramsdale amesema mchezaji mwenzake wa Arsenal na England, Bukayo Saka "hataepuka" kupiga penalti kwenye Kombe la Dunia la Qatar licha ya kukosa moja kwenye fainali ya Euro 2020. (***Mirror***)

### VINICIUS ALIHOFU KUUMIA

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Brazil, Vinicius Junior mwenye umri wa miaka 22 alihofia kupata jeraha kabla ya Kombe la Dunia kwa sababu ya "kuchezewa visivyo " na wapinzani kwenye LaLiga. (***ESPN***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO MAMBO MAGUMU UNITED

Klabu hiyo inajipanga kumchukulia hatua 'kali' kutokana na kauli tata...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imesema itachukua "hatua zinazofaa" baada ya mahojiano ya mshambuliaji wake, Cristiano Ronaldo ambaye alisema "alisalitiwa na klabu".

Fowadi huyo wa Timu ya Taifa ya Ureno alisema "hana heshima" kwa kocha Erik ten Hag na analazimishwa kuondoka hapo Old Trafford.

"Manchester United asubuhi ya leo (juzi) imeanzisha hatua zinazofaa kujibu mahojiano ya hivi karibuni ya Cristiano Ronaldo kwenye vyombo vya habari," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

**Klabu haitatoa maoni zaidi hadi "mchakato huu ufikie mwisho wake".**

Baada ya mahojiano mapana na Piers Morgan kwenye TalkTV, hatima ya Ronaldo ndani ya Manchester United iko mashakani.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 37 atakuwa nahodha wa Ureno kwenye fainali za Kombe la Dunia zinazotarajiwa kufanyika kuanzia leo huko nchini Qatar, na mchezo wao wa ufunguzi wa Kundi H utacheza Alhamisi dhidi ya Ghana.

Nyota huyo hajacheza kwa sababu ya ugonjwa ambao haujatajwa tangu alipokuwa nahodha wa United katika kichapo cha mabao 3-1 dhidi ya Aston Villa katika mchezo uliofanyika Novemba 6, mwaka huu.

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
QATAR
VERSUS
EQUADOR
1 | 3.15
X | 3.00
2 | 2.38

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BALDE AITWA HISPANIA KUMBADILI GAYA



**DOHA,** Qatar

MLINZI wa pembeni wa Barcelona mwenye umri wa miaka 19, Alejandro Balde ameongezwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Hispania kwa ajili ya kushiriki kwenye fainali za Kombe la Dunia baada ya kuumia kwa Jose Gaya.

Beki wa kushoto wa Valencia, Gaya ameichezea Hispania mara 18 baada ya kucheza mechi yake ya kwanza ya kimataifa mwaka 2018, na ulionekana uwezekano wa kuwa naibu nahodha wa La Roja hao, Jordi Alba nchini Qatar.

Hata hivyo, Gaya aliumia kifundo cha mguu akiwa mazoezini Jumatano, na ingawa ripoti za awali zilisema jeraha lake si kubwa, kocha, Luis Enrique ameamua kutojihusisha na hatari yoyote kabla ya michuano hiyo.

Balde alikuwa akijiandaa kuiwakilisha timu ya Hispania chini ya umri wa miaka 21 dhidi ya Japan katika mechi ya kirafiki siku ya Ijumaa, lakini sasa anaweza kushinda mechi yake ya kwanza ya wakubwa kwenye hatua hiyo kubwa zaidi.

Balde alicheza mechi yake ya kwanza Barcelona katika mechi ya kichapo cha Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich Septemba mwaka jana, na amechukua nafasi kubwa katika timu yenye sura mpya ya Xavi msimu huu.

Hispania itaanza kampeni ya Kundi E dhidi ya Costa Rica kwenye Uwanja wa Al Thumama hapo Jumatano, kabla ya kumenyana na Ujerumani katika pambano kubwa siku nne baadaye.

# Pombe marufuku viwanjani Qatar



**DOHA,** Qatar

POMBE hazitauzwa katika viwanja nane vya Kombe la Dunia nchini Qatar, kwa mujibu wa Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Pombe ilipangwa kutolewa "katika maeneo maalumu ndani ya viwanja", licha ya uuzaji wake kudhibitiwa vikali katika nchi hiyo ya Kiislamu.

Wale walio katika maeneo ya biashara ya viwanja kwenye mashindano bado wataweza kununua pombe.

Mabadiliko ya msimamo huo yamefanywa siku mbili kabla ya fainali za Kombe la Dunia kuanza kesho wakati Qatar itakapowakaribisha Ecuador.

"Baada ya majadiliano kati ya viongozi wa nchi wenyeji na FIFA, uamuzi huo umefanywa kulenga uuzaji wa vileo kwa mashabiki.

"Maeneo mengine ya mashabiki na kumbi zilizo na leseni watauziwa, lakini sio ndani ya viwanja vya mpira," ilisema taarifa ya shirikisho hilo.

"Hakuna athari kwa uuzaji wa Bud Zero ambayo itaendelea kupatikana katika viwanja vyote vya Kombe la Dunia la Qatar.

"Mamlaka za nchi mwenyeji na Fifa zitaendelea kuhakikisha viwanja na maeneo ya jirani yanatoa uzoefu wa kufurahisha na heshima kwa mashabiki wote."

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

# SOPU AREJEA DIMBANI AZAM IKIIVAA NAMUNGO

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa Azam FC, Abdul Suleiman 'Sopu' ambaye tangu Oktoba 16 alikuwa nje kutokana na maumivu ya misuli, anatarajiwa kurejea dimbani wakati timu yake itakapoikabili Namungo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Majaliwa ulioko Ruangwa, mkoani Lindi.

Kaimu Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema Sopu yuko fiti na huenda akaonekana katika mechi ya leo pamoja na Malickou Ndoye ambaye amesafiri na kikosi hicho baada ya kutoonekana uwanjani kwa muda mrefu kufuatia majeraha aliyokuwa nayo.

"Mechi dhidi ya Namungo siku zote haiwezi kuwa rahisi, hautakuwa mchezo mdogo hata kidogo, ila tumejidhatiti kushinda na kwa bahati nzuri wachezaji wetu wengi ambao walikuwa majeruhi wamerejea, baadhi wataonekana.

Sopu amerejea kikosini, yupo fiti anaweza kuanza au kuingia kipindi cha pili, Ndoye ambaye naye kwa muda mrefu alikuwa majeruhi naye tumesafiri naye, Prince Dube baada ya kukosekana mechi iliyopita yupo na Idris Mbombo ambaye kwenye mechi iliyopita alipata maheraha madogo lakini naye ni mzima wa afya," alisema Ibwe.

Ofisa huyo alisema kwa sasa Azam iko katika nyakati nzuri ambazo wanaendelea kuzifurahia kwanza kabisa kutokana na matokeo ya mechi zao za ligi, lakini pia upana wa kikosi unaompa fursa panda Kaimu Kocha Mkuu, Kalimangonga Ongalla, kupanga kikosi.

Sopu amekuwa akisumbuliwa na maumivu ya misuli alipoumia katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Akhdar ya Libya iliyochezwa Oktoba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, ambapo licha ya kushinda mabao 2-0, iliondoshwa kwa jumla ya mabao 3-2.

Iwapo Azam itashinda mechi ya leo, itakuwa ni ya sita mfululizo tangu ilipoanza kunolewa na Kalimangonga baada ya uongozi kumfurusha kazi aliyekuwa Kocha Mkuu, Mfaransa Denis Lavagne.

Kabla ya mechi ya jana usiku kati ya Simba dhidi ya Ruvu Shooting, Azam FC yenye pointi 26 ilikuwa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania wakati Namungo yenye pointi 15 iko nafasi ya nane.



Bondia, Swahibu Ramadhan (kushoto) akitambiana na mpinzani wake, Emmanuel Kitimtim (kulia) kuelekea katika pambano lao la Dar Boxing Derby litakalofanyika leo kwenye Uwanja wa Kinesi, Dar es Salaam. **PICHA: SAADA AKIDA**

## Yanga, Dodoma Jiji hesabu zakamilika

INATOKA UK. 24

bao 2-0, sasa tumerudi kujiandaa dhidi ya Yanga mchezo ambao tunatarajia kuuchezea ugenini Uwanja wa Liti, Singida kutokana na uwanja wetu kufanyiwa maboresho.

"Tumefanya mazoezi asubuhi na mchana katika uwanja wetu wa mazoezi, licha ya sisi kuwa wenyeji lakini bado tunacheza ugenini, tuwaombe radhi mashabiki wetu na wajitokeze kwa wingi kuja kutusapoti. Dodoma Jiji ni timu kubwa popote tunapokwenda kucheza tutapata matokeo, huu ni moja ya michezo muhimu katika mwezi huu, tutapambana ili tupate ushindi. Tunawaheshimu Yanga lakini uwanjani tunacheza watu 11 na dakika 90 ndizo zitakazoamua, tunakwenda kushinda, ng'ombe atakapogeukia ndipo atakapochinjiwa, tunaenda kustopisha 'unbeaten'," alitamba kiongozi huyo.

Aliongeza kikosi chao kitawakosa nyota wake wawili ambao ni Jimmy Shoji ambaye amefanyiwa upasuaji wa goti na Abubakari Nalema aliyeumia mguu wa kushoto.

INATOKA UK. 24

## Simba: Ubingwa Ligi Bara lazima

Alisema pia katika kuongeza nguvu ndani ya benchi la ufundi, wanatarajia kumtambulisha kocha mkuu mpya atakayesaidiana na Juma Mgunda katika kipindi hiki ambacho nahodha wao wa zamani, Selemani Matola, amekwenda kushiriki kozi leseni A.

"Timu imekaa muda mrefu bila ya kuwa na kocha wa viungo, kocha wa makipa, na Kocha Mkuu, nafasi ambayo aliikaimu Mgunda, baada ya kikao cha bodi, hilo limeisha na tunasubiri utambulisho rasmi wa Kocha Mkuu muda wowote ndani ya hizi siku mbili," aliongeza.

Alieleza ujio wa makocha hao utaongeza nguvu ndani ya timu yao na wanaamini wachezaji watarejea katika utimamu wa mwili imara tayari kupambana na ushindani kutoka kwa timu pinzani.

"Timu inakuwa imara na itarejea kwenye ubora wake uliozoeleka, tunaamini tutakuwa timu imara zaidi na makali yetu yataonekana," alisema Ahmed.

Pia alisema kikao hicho cha juu kilijadili maendeleo ya ujenzi wa uwanja wao wa Mo Simba Arena na kusema hatua ya pili inatarajiwa kuanza hivi karibuni huku uzio ukiwa kwenye hatua za mwisho kukamilika.


MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 20/11/2022


| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 3461 | Ufa vs Rubin Kazan | 14.63 | 4.88 | 1.21 |
| 12:15 | 4545 | Banik Ostrava B vs Znojmo | 1.24 | 6.03 | 7.98 |
| 13:00 | 5917 | FC Minaj vs FC Metalist Kharkiv | 3.06 | 3.25 | 2.15 |
| 13:30 | 4392 | Nakhon Ratchasima vs Chonburi | 2.87 | 3.36 | 2.20 |
| 13:30 | 5081 | Bodrumspor vs Tuzlaspor | 1.71 | 3.58 | 4.26 |
| 14:00 | 1727 | Carrarese vs Olbia Calcio | 1.85 | 3.36 | 4.31 |
| 14:00 | 1891 | Celta B vs Rayo Majadahonda | 1.79 | 3.21 | 4.37 |
| 14:00 | 2098 | Suphanburi vs Krabi FC | 1.31 | 4.67 | 7.98 |
| 14:00 | 2410 | Lampang vs Lamphun Warrior | 2.35 | 3.26 | 2.72 |
| 14:00 | 3456 | Numancia vs CE Sabadell | 2.16 | 3.07 | 3.21 |
| 14:00 | 4900 | Amorebieta vs CF La Nucia | 2.03 | 3.05 | 3.59 |
| 15:00 | 4735 | Naesby BK vs AB Taarnby | 1.61 | 3.89 | 4.47 |
| 15:00 | 5942 | Ratchaburi vs Bangkok Glass | 3.26 | 3.35 | 2.02 |
| 15:30 | 1267 | Glentoran Belfast vs Cliftonville Belfast | 1.78 | 3.46 | 4.00 |
| 15:30 | 1372 | Slovakia vs Chile | 2.83 | 3.28 | 2.49 |
| 16:00 | 1101 | FC Dynamo-Makhachkala vs Volgar Astrahan | 2.29 | 3.02 | 3.02 |
| 16:00 | 1492 | FC Veria vs Apollon Larisas | 1.25 | 5.25 | 8.94 |
| 16:00 | 2289 | Caykur Rizespor vs Boluspor | 2.01 | 3.30 | 3.35 |
| 16:00 | 2848 | Norway vs Finland | 1.65 | 3.68 | 5.45 |
| 16:00 | 4237 | Eyupspor vs Goeztepe | 1.63 | 3.68 | 4.65 |
| 16:00 | 5298 | North Macedonia vs Azerbaijan | 1.65 | 3.79 | 5.26 |
| 16:15 | 5784 | FC Vaduz vs Lausanne-Sport | 2.77 | 3.54 | 2.19 |
| 16:30 | 3422 | Viterbo Calcio vs Crotone | 4.69 | 3.60 | 1.73 |
| 16:30 | 4587 | Dordrecht vs Willem II Tilburg | 4.15 | 3.86 | 1.71 |
| 16:30 | 4702 | Latina vs Juve Stabia | 2.21 | 3.15 | 3.35 |
| 16:30 | 5212 | Alessandria vs AC Siena | 3.59 | 3.14 | 2.11 |
| 17:00 | 1714 | Slovenia vs Montenegro | 2.13 | 3.24 | 3.54 |
| 17:00 | 2063 | FC Krasnodar II vs Ska Energiya | 4.18 | 3.54 | 1.73 |
| 17:00 | 2508 | Oman vs Belarus | 3.13 | 3.33 | 2.27 |
| 17:00 | 2971 | Luxembourg vs Bulgaria | 2.46 | 3.28 | 2.87 |
| 17:00 | 3465 | FC Goa vs ATK Mohun Bagan | 3.05 | 3.34 | 2.11 |
| 18:00 | 4979 | Cordoba vs CD Linares | 1.45 | 3.99 | 6.23 |
| 18:15 | 3079 | FC Andorra vs Lugo | 1.78 | 3.31 | 4.64 |
| 19:00 | 5813 | Qatar vs Ecuador | 3.15 | 3.00 | 2.38 |
| 19:00 | 5928 | Sakaryaspor vs Bandirmaspor | 2.68 | 3.17 | 2.43 |
| 19:30 | 4420 | Lucchese vs Gubbio | 2.80 | 3.05 | 2.60 |
| 19:30 | 4553 | Israel vs Cyprus | 1.53 | 3.98 | 6.44 |
| 20:00 | 5931 | Venezuela vs Syrian Arab Republic | 1.68 | 3.63 | 5.24 |
| 20:15 | 2570 | Real Sociedad C vs CD Arnedo | 1.88 | 3.25 | 3.83 |
| 21:00 | 2443 | Deportivo La Coruna vs Leonesa | 1.49 | 3.89 | 5.84 |
| 21:00 | 2906 | Covilha vs Gil Vicente | 4.58 | 3.51 | 1.68 |
| 21:00 | 3169 | Racing Santander vs Burgos | 2.39 | 2.78 | 3.32 |
| 21:00 | 5959 | Eibar vs Alaves | 2.02 | 3.17 | 3.71 |
| 21:30 | 5208 | Moldova vs Romania | 6.50 | 4.16 | 1.50 |
| 22:00 | 2226 | CF Estrela vs Benfica | 14.00 | 7.00 | 1.16 |
| 22:00 | 5946 | Malta vs Ireland | 7.87 | 4.54 | 1.40 |
| 22:15 | 4499 | Hungary vs Greece | 2.24 | 3.23 | 3.28 |
| 22:45 | 5181 | Austria vs Italy | 3.49 | 3.19 | 2.18 |
| 23:00 | 2602 | Levante vs Las Palmas UD | 2.25 | 3.07 | 3.22 |
| 23:15 | 5396 | Pacos Ferreira vs Casa Pia Atletico | 3.30 | 3.15 | 2.23 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Novemba 20, 2022

Nipashe

Ronaldo mambo magumu United UKURASA 21



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kulia), akisalimiana na winga wa Singida Big Stars, Deus Kaseke mara baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyozikutanisha timu hizo mbili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Alhamisi. Yanga ilishinda mabao 4-1. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA, DODOMA JIJI HESABU ZAKAMILIKA

## ●●● Nabi atamba mbinu na mikakati ya kuendeleza dozi imetimia baada...

**Saada Akida na Hadija Mngwai**

KATIKA kuhakikisha wanaendeleza rekodi yao ya 'Unbeaten', Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amesema kikosi chake kiko imara kutokana na mbinu na mikakati anayowapa kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika kila mechi wanayocheza.

Kikosi cha Yanga kimeondoka jijini, Dar es Salaam leo asubuhi kuelekea Singida kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa CCM Liti mkoani humo.

Dodoma Jiji inatumia uwanja huo kufuatia dimba la CCM Jamhuri kufungiwa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB) kwa lengo la kuufanyia marekebisho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema hawana muda mrefu wa kufanya mazoezi kwa sababu ya mechi kuwa karibu karibu, hivyo anatumia muda mrefu kuzungumza na kuwaandaa wachezaji wake kisaikolojia.

Nabi alisema kikubwa ambacho anakifanya wanapopata muda ni kurekebisha madhaifu yao na kuboresha idara ambazo ziko imara ili kuendelea kufanya vizuri zaidi.

"Baada ya kuibuka na ushindi mnono dhidi ya Singida Big Stars niliwaambia wachezaji wangu haya matokeo yamepita na sasa tuwekeze nguvu zetu na akili katika mechi yetu ijayo ili tuendelee kufanya vizuri. Kama nilivyowaambia ubingwa hatuwezi kuupata bila ya kujitoa kwa kila mmoja kupambana kwa ajili ya kufikia malengo ya kile tunachokitarajia," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza jambo zuri kwao ni kipa, Diarra Djigui kurejea na kuungana na wachezaji wenzake katika mazoezi ya kujiandaa na mechi hiyo ambapo walipeleleza Dodoma Jiji ilipokuwa ikicheza na KMC FC hivi karibuni.

"Timu ina malengo, tunaamini tumefanya maandalizi ya kutosha kuhakikisha tunashinda mchezo huo, wenzetu pia wanajiandaa, hivyo kutakuwa na mchezo mgumu kwa sababu tulikuwa uwanjani kuona jinsi ambavyo wanacheza. Tunajua wapinzani wetu si timu nyepesi," alisema Nabi.

Aliongeza ligi hiyo wanayoshiriki ni ngumu kwa sababu kila timu inafanya maandalizi imara kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mechi zote na wataingia dimbani huku wakiwaheshimu wapinzani wao.

Wakati huo huo, mabosi wa Dodoma Jiji wametamba kikosi chao kiko imara na tayari kuwasimamisha Yanga ambao pia ndio mabingwa watetezi wa ligi hiyo.

Ofisa Habari wa Dodoma Jiji, Moses Mpunga, alisema wanatambua ukubwa wa Yanga lakini wao wamejipanga kuondoka na pointi zote tatu katika mchezo huo na kuendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi.

"Tunashukuru Mungu tumerudi salama Dodoma baada ya michezo yetu ya Dar es salaam, tulifungwa dhidi ya Azam 1-0 halafu tukashinda dhidi ya KMC ma-

INAENDELEA UK. 23

# Simba: Ubingwa Ligi Bara lazima

**Na Saada Akida**

BODI ya Wakurugenzi ya Klabu ya Simba iliyoko chini ya Mwenyekiti wake, Salim Abdallah 'Try Again' ilikutana jijini, Dar es Salaam juzi na kufikia makubaliano ya kuhakikisha timu zake, Simba na Simba Queens zinapata mafanikio katika msimu huu unaoendelea.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema miongoni mwa vitu vilivyojadiliwa ni kuwapo na mipango na mikakati ya timu yao kufanya vizuri katika Ligi Kuu Tanzania Bara, hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayoanza Februari mwakani na michuano ya Kombe la FA.

Ahmed alisema klabu inataka kuona inajiimarisha na hatimaye inarejesha mataji yote ambayo iliyapoteza katika msimu uliopita.

"Bodi imejadili mambo mengi kuhusu mwenendo wa timu yetu ya Simba na Simba Queens kuelekea msimu mpya wa Ligi ya Soka ya Wanawake inayotarajiwa kuanza Desemba 6, mwaka huu, tutahakikisha tunatetea ubingwa wetu," alisema Ahmed.

Aliongeza malengo yao ni kuona timu zote mbili zinapata matokeo mazuri katika kila mechi zilizopo mbele yao kwa kupambana ili wafikie malengo yao.

"Uongozi unaendelea na majukumu yake ikiwamo hivi karibuni tumetambulisha makocha wawili, kocha wa viungo, Kelvin Ndlomo kutoka Afrika Kusini na kocha wa makipa, Chlouha Zakaria ambaye ni raia wa Morocco," alisema ofisa huyo.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >